# Jarida la BUNGE

ISSN-085-6046 TOLEO LA KUMI NA MOJA JANUARI, 2026



# "RAIS Dkt. Samia Afungua Bunge la 13"

## Yaliyomo




Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu achaguliwa kuwa Spika wa Bunge la 13 UK 17









RAIS Dkt. Samia Afungua Bunge la 13 UK 02

Dkt. Mwigulu Nchemba ateuliwa kuwa Waziri Mkuu UK 20

Mheshimiwa Daniel Sillo achaguliwa Naibu Spika wa Bunge la 13 UK 27


*Scan hii Code kusoma na kupakua jarida hili*

# Dibaji




## Bodi ya Uhariri

**Mwenyekiti**
Ndg. Baraka Leonard

Makamu Mwenyekiti
Ndg. Zuhura Mtatifikolo

**Wajumbe**
Ndg. Athuman Hussein, *ndc*
Ndg. Hanifa Masaninga
Ndg. Abdallah Hancha
Ndg. Chacha Nyakega

**Mhariri**
Ndg. Lawrence Raphaely

**Mhariri Msaidizi**
Ndg. Debora Sanja



Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA.
Nukushi: +255 26234218
Simu: +255 26 232276-5
Barua Pepe: cna@bunge.go.tz


*Scan hii Code kupakua na kusoma jarida hili*

Ndugu Msomaji,

Nakukaribisha kwenye Jarida la Bunge Toleo la Kumi na Moja ambalo lina habari kuhusu Ufunguzi wa Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha Jarida hili lina habari kuhusu Uchaguzi wa Spika wa Bunge, Uchaguzi wa Naibu Spika wa Bunge, Kuthibitisha Uteuzi wa Waziri Mkuu, Viapo vya Wabunge na Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano ya CPA Kanda ya Afrika.

Pia kuna makala mpya kuhusu Uwajibikaji wa Mbunge na Utaratibu rasmi wa Wabunge Walio Wachache Bungeni katika Mabunge ya nchi za kidemokrasia.

Kwa upande mwingine kuna muendelezo wa makala zinazochambua kwa kina kuhusu Umuhimu wa Kamati za Kudumu za Bunge na Usimamizi wa Kibunge wa Matumizi ya Fedha za Umma.

Pamoja na hayo masuala mengine ambayo yameandikwa katika Jarida hili ni pamoja na makala kuhusu Mchango wa Hayati Job Yustino Ndugai katika historia ya Bunge la Tanzania na Historia ya Spika wa Tatu wa Bunge baada ya Uhuru, Hayati Chifu Erasto Mang'enya.

Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la Bunge Toleo la Kumi na Moja.

Ndugu Baraka Leonard
Katibu wa Bunge.

# Yaliyomo



UK 02
RAIS Dkt. Samia Afungua Bunge la 13


UK 17
Mhe. Mussa Azzan Zungu achaguliwa kuwa Spika wa Bunge la 13


UK 20
Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba ateuliwa kuwa Waziri Mkuu


UK 25
Bunge la 13 laanza, Wabunge waapishwa.


UK 27
Mhe.Daniel Sillo achaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la 13


UK 29
Usimamizi wa Kibunge wa Fedha za Umma


UK 33
Chifu Erasto Andrew Mbwana Mang'enya


UK 38
Job Yustino Ndugai: Ameacha Alama Isiyofutika Katika Historia Ya Bunge La Tanzania


UK 43
Mkataba Wasainiwa Ujenzi wa Hoteli ya CPA Dodoma


UK 45
Utaratibu Rasmi wa Wabunge walio Wachache Bungeni katika Mabunge ya nchi za Kidemokrasia


UK 48
Uwajibikaji wa Mbunge


UK 52
Diplomasia ya Kibunge yaimarishwa kupitia Mkutano wa 68 wa CPC na Mkutano wa 151 wa IPU


UK 54
Umuhimu wa Kamati za Bunge katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge



# RAIS Dkt. Samia Afungua Bunge la 13

- **Asisitiza Umoja wa Kitaifa**
- **Aeleza Mwelekeo wa Serikali yake**

*Na. Lawrence Raphaely*

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amelihutubia na kulifungua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 14, 2025 Jijini Dodoma.**

Akizungumza kuhusu wajibu wake wa Kikatiba wa kulifungua Bunge, Mhe. Rais alisema kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 91, (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana dhima ya kulifungua rasmi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Ni kwa msingi huo, leo nipo hapa kulihutubia Bunge ili kutimiza matakwa ya Ibara hiyo ya Katiba," alisema.

### Azungumzia vurugu zilizojitokeza wakati wa Uchaguzi Mkuu

Akilihutubia Bunge hilo, Mhe. Rais alianza kwa kuzungumzia hali iliyotokea baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 29, 2025 ambapo aliwaomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na



wageni waalikwa waliohudhuria tukio la ufunguzi wa Bunge kusimama kwa dakika moja kuomboleza na kuwaombea waliopoteza maisha wakati wa vurugu zilizotokea siku ya uchaguzi huo.

"Mimi binafsi nimehuzunishwa sana na tukio lile. Natoa pole kwa familia zote zilizopoteza wapendwa wao, na tunamuomba Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani. Aidha, kwa majeruhi tunawaombea wapone kwa haraka, na kwa wale waliopoteza mali zao tunawaomba wawe na stahamala na uvumilivi," alisema.

Kuhusu hali hiyo, Mhe. Rais alisema Serikali imechukua hatua ya kuunda Tume ya kuchunguza yaliyotokea kujua kiini cha tatizo.

Alisema taarifa ya Tume hiyo itaongoza katika kujielekeza kwenye mazungumzo ya kuleta maelewano na amani.

Aliongeza kuwa vurugu na uvunjifu wa amani uliojitokeza wakati wa Uchaguzi Mkuu ulisababisha uharibifu wa mali, kupoteza maisha na kuhatarisha usalama wa nchi.

"Tunapoenda mbele, niwasihi sana Watanzania tuongozwe na dhamira ya maelewano, ushirikishwaji, kujirekebisha na umoja," alisema.

Aliwaasa pia vijana watambue kwamba nchi imejengwa kwenye misingi ya amani na utulivu wa kisiasa na kwamba wasikubali hata siku moja kushawishiwa kuichoma.

"Msikubali kukata tawi la mti ambalo mmeukalia. Hili nawaomba mlikatae kwa nguvu zenu zote. Ninyi ndio walinzi na wajenzi wa Taifa hili, nawasihi kamwe msije kuwa wabomoaji wa Taifa lenu," alisema.

### Atoa msamaha kwa vijana waliofanya vurugu wakati wa Uchaguzi

Rais Dkt. Samia wakati akilihutubia na kulifungua Bunge la 13 aliviagiza vyombo vinavyosimamia sheria hususan Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuangalia kiwango cha makosa yaliyofanywa na vijana walioshiriki katika vurugu wakati wa uchaguzi na kwa wale ambao wanaonekana walifuata mkumbo na hawakudhamiria kufanya uhalifu wawafutie makosa yao.

Alisema kuna wakati vijana hufuata mkumbo wa uhalifu kwa ushabiki, na anatambua kwamba kuna vijana wengi waliokamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya uhaini ambao hawakujua wanachokifanya.

"Nikiwa mama na mlezi wa Taifa hili, ninavielekeza vyombo vya sheria na hasa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuangalia kiwango cha makosa yaliyofanywa na vijana wetu. Kwa wale ambao wanaonekana walifuata mkumbo na hawakudhamiria kufanya uhalifu wawafutie makosa yao," alisema.

"Ninatoa msamaha huo kwa sababu, hata maneno ya Mungu katika Kitabu cha Luka Sura ya 23:34 yanasema, na hapa nanukuu: "Yesu akasema, Baba uwasamehe kwa kuwa hawajui watendalo," alisema.

Mhe. Rais aliwaasa pia wananchi wajifunze kutokana na mapito waliyopitia kwani Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya kidemokrasia, ila, demokrasia kamili inaweza kutafsiriwa kwenye mitazamo tofauti.

"Kama Taifa tunaendelea kujifunza na kujirekebisha. Hivyo basi, sote kwa umoja wetu tunapaswa tuitumie fursa hii tuendelee kujifunza, tujirekebishe na tukubaliane jinsi ya kuiendesha nchi yetu kidemokrasia kwa kuzingatia tamaduni, mila na desturi zetu na sio za kuletewa," alisema.

### Marekebisho ya Katiba

Akizungumza kuhusu marekebisho ya Katiba, Mhe. Rais alisema Serikali yake italifanyia kazi suala





**Kuelekea 2030, tutafanya mageuzi ya mashirika ya umma ili kuboresha ufanisi, uwazi na tija. Tunataka kuongeza sio tu gawio ambalo Serikali inapokea, lakini pia kufikia lengo la Mashirika na Taasisi za Umma kuchangia angalau asilimia 10 ya mapato yote yasiyo ya kodi**

la mabadiliko ya Katiba kwa kuanza na Tume ya Usuluhishi na Maelewano.

"Kama tulivyoagizwa na Ilani ya CCM ya mwaka 2025 hadi 2030, moja ya hatua itakayotufikisha kwenye maelewano hayo ni marekebisho ya Katiba yetu," alisema.

Aliongeza kuwa moja ya kipaumbele cha Serikali atakayounda ni kuendelea kuudumisha, kuimarisha na kuuenzi Muungano.

"Tutaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha tunatatua changamoto za Muungano kila zinapojitokeza," alisisitiza.

### Mambo atakayoanza nayo ndani ya siku 100

Akianisha mambo ambayo Serikali yake itaanza nayo ndani ya siku 100, Mhe. Dkt. Samia alisema suala la kwanza linahusu utumishi na utawala bora, ambalo ni suala la uundwaji wa Serikali.

"Niliwaahidi wananchi kuwa Serikali nitakayoiunda itawajibika na kuendelea na mageuzi ya sera zinazogusa maslahi na ustawi wa maisha ya wananchi moja kwa moja," alisema.

Alisema kwa muktadha huo, ni lazima viongozi wa Serikali kwa ngazi zote, kuanzia Mawaziri hadi Maafisa Tarafa, wawe karibu na wananchi ili kuweza kufahamu changamoto zao na kuwajibika kwao.




"Kwa kuwa ahadi tulizotoa ni nyingi, matamanio ni mengi, matarajio ni makubwa, na muda wa kuyatimiza haya ni mchache, tutaongeza kasi ya utekelezaji wa mipango ya Serikali ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea," alisema.

Alisema ameyagusia hayo mapema kwa watendaji waliopo Serikalini, wakiwemo Makatibu Wakuu, na wale atakaowateua kwa ajili ya kujitayarisha kisaikolojia na kujipanga vyema kufanikisha malengo hayo.

"Wananchi wanahitaji mabadiliko chanya kwa maendeleo. Watendaji msipobadilika, kuendana na matarajio ya wananchi, tutawabadilikia," alisema.

Sambamba na hayo alisema ili kuhakikisha wananchi wananufaika na rasilimali za nchi pamoja na kupata huduma wanazostahili, uongozi wake utaelekeza jitihada zake kwenye mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi, ubadhirifu, uzembe, ukosefu wa nidhamu na ukosefu maadili.

"Ni lazima tudhibiti wachache wanaotaka kuturudisha nyuma kwa kuendekeza maslahi binafsi. Aidha, ili kuimarisha uwajibikaji Serikalini, tutaendelea kutekeleza programu za maboresho ya utumishi wa umma, ikiwemo matumizi ya mifumo ya upimaji wa utendaji kazi," alisema.

"Wajibu huenda na haki, au haki huambatana na wajibu. Hivyo basi, pamoja na kuwataka



watumishi wa umma kuwajibika ipasavyo, tutaendelea kuboresha maslahi yao kadri uchumi utakavyoruhusu," alisema.

Vilevile, alisema Serikali yake itaimarisha uwajibikaji na utendaji wa mashirika ya umma.

"Kuelekea 2030, tutafanya mageuzi ya mashirika ya umma ili kuboresha ufanisi, uwazi na tija. Tunataka kuongeza sio tu gawio ambalo Serikali inapokea, lakini pia kufikia lengo la Mashirika na Taasisi za Umma kuchangia angalau asilimia 10 ya mapato yote yasiyo ya kodi," alisema.

Kuhusu Mahakama, Mhe. Rais alisema Serikali yake itaendelea kuwezesha Mahakama kwa majengo, vitendea kazi, watumishi pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA.

Pia alisema Serikali yake itasimamia utekelezaji kamili wa mapendekezo ya Tume ya Rais ya kuangalia namna ya kuboresha Taasisi za Haki Jinai.

"Tutaendelea kufanya mageuzi na maboresho katika taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya Haki Jinai ili ziweze kukabiliana na vitendo vyote vya uhalifu," alisema.

Suala lingine ambalo aliahidi kulifanyia kazi ndani ya siku mia moja ni ahadi ya kutoa ajira kwa fani za Sekta ya Afya na Elimu.

"Leo ikiwa ni siku ya kumi na mbili tangu muhula huu wa pili wa Awamu ya Sita uanze, tayari tumeshatangaza nafasi za ajira 7,000 za walimu na nafasi za ajira 5,000 za watumishi wa afya," alisema.

Aliongeza kuwa hatua hiyo ni ya mwanzo katika kujibu kiu ya wananchi ya kuboresha huduma za afya na elimu.

"Katika hatua nyingine, tunajiandaa kuanza kwa majaribio ya Bima ya Afya kwa Wote. Serikali itakuja kwenu Waheshimiwa Wabunge na mapendekezo ya namna ya kufanikisha majaribio hayo, na niwaombe muunge mkono mapendekezo hayo ambayo yatakuwa mwanzo wa mageuzi katika upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watu wote nchini," alisema.

Pia alisema ameshaelekeza Wizara ya Afya kusimamia maelekezo ya kutozuiwa maiti kwenye



**Tume ya kuanzisha Mazungumzo ya Maridhiano na Upatanishi na kuandaa mazingira ya kuanza kwa Mchakato wa mabadiliko ya Katiba.**

**Suala lingine ambalo Mhe. Rais alilizungumzia**

vituo vya kutolea huduma za afya, wakati familia zikiendelea na taratibu za kulipa deni la matibabu kwa njia zinazolinda utu wao.

"Niseme kwamba, ni kupitia mpango huu wa bima ya afya, kadhia hii inakwenda kukomeshwa. Kwa sababu gharama za matibabu zitalipwa na bima ya anayetibiwa. Niwasihi wananchi wote kuweka kipaumbele kwa afya zetu, kwa kila mmoja wetu kuwa na bima ya afya pamoja na wanaomtegemea," alisema.

Suala lingine ambalo Mhe. Rais alilizungumzia ni Tume ya kuanzisha Mazungumzo ya Maridhiano na Upatanishi na kuandaa mazingira ya kuanza kwa mchakato wa mabadiliko ya Katiba.

Alisema kutokana na uvunjifu wa amani uliotokea nchini wakati wa Uchaguzi Mkuu kutahitajika kufanya tathmini ya kina ili kujua kiini na sababu ya kadhia hiyo, na ndipo Tume ya Maridhiano iundwe.

Alifafanua kuwa katika muhula kwa kwanza wa Awamu ya Sita, Serikali ilianzisha falsafa ya R4 ili kuliunganisha Taifa ambapo ilionesha utayari wakati wote katika kuleta maridhiano.

"Serikali ilinyoosha mkono kuwavuta na kuwakaribisha Vyama vya Siasa, Vyama vya Kijamii, Sekta binafsi na hata Jumuiya za Kimataifa, ili kwa pamoja tuijenge Tanzania. Waheshimiwa Wabunge, mkono huo wa urahimu ulileta matumaini kwa nchi, kabla ya baadhi ya wadau kuamua kuuachilia au kuutupa mkono huo," alisema.

Aliongeza kuwa kwa kuwa wananchi wa Tanzania wamempa ridhaa ya kuendelea kuiongoza nchi hatachoka kunyoosha tena mkono wa maridhiano.

"Ni matumaini yangu kuwa wadau wa kisiasa wataupokea kwa dhati mkono wa maelewano, ili kwa pamoja tujenge mazingira muafaka kwa maendeleo ya Taifa letu. Tutajifunza kutokana na makosa na mapungufu ya taasisi zetu za kidemokrasia," alisema.



**Ili kuhakikisha vijana wanapata nafasi ya kushiriki katika kujenga mustakabali mwema wa Taifa letu, tutaweka kipaumbele kwenye ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya maendeleo yao,**

Mhe. Rais Dkt Samia

Jambo lingine ambalo Mhe. Rais alizungumzia ni kuhusu vijana ambapo alisema asilimia 60 ya Watanzania ni vijana hivyo Serikali yake itaweka kipaumbele kwenye sera na programu zitakazopanua fursa za kiuchumi, kutengeneza kazi na ajira kwa vijana.

"Ili kuhakikisha vijana wanapata nafasi ya kushiriki katika kujenga mustakabali mwema wa Taifa letu, tutaweka kipaumbele kwenye ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya maendeleo yao," alisema.

Aliongeza kuwa anatambua kwamba kumekuwa na majukwaa mengi ya kuwafikia vijana ila bado shughuli zao zinafifishwa na masuala ya kisiasa, na majukwaa hayo kupoteza malengo na mvuto kwa vijana.

Kwa mukhtadha huo, Mhe. Rais alisema wamepanga kuwa na Wizara kamili itakayoshughulika na mambo ya vijana, badala ya kuwa na Idara ndani ya Wizara yenye mambo mengi.

"Vilevile, ninafikiria kuwa na washauri wa masuala ya vijana ndani ya Ofisi yangu," Mhe. Rais alisema.

Jambo lingine ambalo Mhe. Rais alisema litatekelezwa ndani ya siku 100 za awali za utawala wake ni kuongeza mitaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi za vijana na wanawake kwa kutenga shilingi bilioni 200.

"Serikali inaendelea kuangalia njia nzuri ya kuimarisha mfuko huo kwa lengo la kuongeza

ufanisi kwa walengwa. Aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi, tutaanzisha madirisha ya uwekezaji kwa vijana," alisema.

## Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo

Akizungumzia masuala mengine ambayo Serikali yake itafanyia kazi ndani ya miaka mitano katika kuendeleza ukuaji wa uchumi Mhe. Rais alisema katika kipindi hicho utekelezaji utafanyika wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 hadi 2050.

"Tukilenga kujenga Taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Dira mpya imeweka vigezo vya kuchagua sekta na maeneo ya kupewa kipaumbele yaliyobainishwa kwenye andiko la Dira yenyewe. Kati ya mikakati itakayofanyiwa kazi ni kuwekeza zaidi kwenye sekta zinazoajiri watu wengi na miongoni mwa sekta hizo ni kilimo, utalii, viwanda, ujenzi na madini," alisema.

Alisema malengo ya kiuchumi ni kupandisha kasi ya ukuaji wa uchumi kutoka asilimia 5.6 ya sasa hadi zaidi ya asilimia saba kuelekea mwaka 2030.

Aliongeza kuwa ukuaji huo utaiwezesha Serikali kuboresha huduma za kijamii na kujenga miundombinu wezeshi ya kiuchumi.

"Tutaimarisha masoko ya mitaji kwa kuhamasisha uwekezaji wa ndani, na kutumia rasilimali zetu kama madini kudhamini mikopo ya uwekezaji, badala ya kuweka mzigo mkubwa kwenye Deni la Taifa. Mwelekeo wetu ni kukua kwa pamoja kwa uchumi unaogusa maisha ya mtu mmoja mmoja na uchumi jumla," alisema.

## Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI)

Akizungumza kuhusu kuboresha mazingira ya biashara hapa nchini, Mhe. Rais alisema utekelezaji utafanyika wa mapendekezo ya Tume aliyounda ya kuboresha mifumo ya kodi nchini ili kuwapatia wafanyabiashara wepesi katika kufanya biashara zao.



"Tutaendelea kuweka nguvu zaidi kudhibiti mfumuko wa bei za bidhaa ambayo ni hatua muhimu katika kupunguza gharama za maisha kwa wananchi. Pia tutaweka motisha kwa viwanda vya ndani ili viweze kuzalisha kwa gharama nafuu na kuuza kwenye soko la ndani na nje," alisema.

Mbali na hilo, Mhe. Rais alisema fursa mahsusi zitatolewa za kuhamasisha vijana na wamiliki wa biashara ndogo kupata elimu ya biashara na kuweza kujisajili katika Mfumo wa Kielektroniki wa Manunuzi ya Serikali.

Vilevile, alisema programu maalum za mafunzo ya ufundi stadi kupitia vyuo vya ufundi stadi (VETA) zitatolewa na pia programu hizo zitaunganishwa na miradi ya mikakati kama reli ya kisasa (SGR), uendelezaji wa bandari, uchumi wa buluu, madini na gesi ili vijana hawa wapate uzoefu na waweze kuajirika.

"Serikali itaanzisha kanda za kuendeleza ujuzi zitakazowawezesha vijana kupata ujuzi unaohitajika katika makampuni ya sekta binafsi, na kuangalia uwezekano wa kutoa vivutio maalum kwa makampuni yatakayotoa nafasi nyingi za ajira kwa vijana," alisema.

Sambamba na hayo, Mhe. Rais alisema mikopo ya asilimia 10 ya makusanyo ya halmashauri itapitiwa upya ili kuboresha upatikanaji wa mikopo hiyo kwa walengwa.

"Matamanio yangu ni kuona ifikapo mwaka 2030, tuwe tumetengeneza wawekezaji vijana ambao watatoa ajira kwa vijana wenzao," alisema.

Katika hatua nyingine, Mhe. Rais alisema kipaumbele kitatolewa katika suala la kutenga maeneo ya biashara kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ili Serikali iwatambue na kuwarasimisha ili waweze kufanya kazi zao bila bughudha na wachangie kwenye Pato la Taifa.

"Kwa rasilimali ambazo nchi yetu imebarikiwa na nguvu kazi kubwa tuliyonayo, ninaamini tunaweza kabisa kujipanga na kufikia lengo hilo. Kwa kufanya hivyo, ndio tutafikia lengo letu la kuzalisha ajira milioni 8.5 katika sekta mbalimbali ifikapo mwaka 2030," alisema.

### Huduma za Kijamii

Kwa upande wa huduma za kijamii, Mhe. Rais alisema azma ya Serikali ni kufikia asilimia 100 ya upatikanaji wa maji safi, salama na uhakika.

"Hivyo tunakwenda kuongeza nguvu ili kuyafikia yale maeneo machache ambayo upatikanaji wa maji bado ni changamoto. Katika miaka mitano ijayo, tutakamilisha ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji ambayo itategemea maji kutoka Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa," alisema.

Aidha alisema miradi mikubwa ya maji inayoendelea ikiwemo miradi ya maji katika miji 28 itakamilishwa.

Kuhusu sekta ya afya, Mhe. Rais alisema mbali na masuala ya Bima ya Afya kwa Wote na ongezeko la ajira za watumishi wa afya, ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati zinazojengwa kote nchini utakamilishwa.

Pia alisema Serikali yake imejipanga kujenga hospitali kubwa ya Kitaifa ya magonjwa ya mlipuko ambayo itajengwa mkoani Kagera.

"Vilevile, tutajielekeza katika kuongeza uwezo wa uzalishaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kupunguza uagizaji na kupunguza gharama za matibabu. Katika hili, tutavihakikishia viwanda vya ndani soko la uhakika kupitia Bohari ya Dawa (MSD)," alisema.

Kwa upande wa elimu, Mhe. Rais alisema katika miaka mitano ijayo utekelezaji kamili wa maboresho ya Sera ya Elimu inayosisitiza elimu ujuzi utafanyika.

"Tutaendelea kuweka mkazo zaidi kwenye masomo ya sayansi na hisabati (STEM). Azma yetu ni kuongeza wanasayansi wabobezi katika eneo la sayansi ya data, akili unde, sayansi ya kompyuta na teknolojia za viwanda," alisema.

Alisema pia utekelezaji utafanyika wa mpango wa kuhakikisha kuwa kila Wilaya ina Chuo cha VETA chenye vifaa stahiki vya mafunzo kwa vitendo.

"Tunaenda kuwekeza zaidi pia kwenye miundombinu ya shule za awali, msingi na sekondari mpya pamoja na kuongeza madarasa kwenye shule," alisema.

### Sekta ya Kilimo

Kuhusu sekta ya kilimo, Mhe. Rais alisema katika miaka mitano ijayo, malengo ni kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa mazao ya mahindi, mchele na mbogamboga Barani Afrika.

"Tutafanya hivyo kwa kujielekeza kwenye kilimo cha kisasa kwa kuongeza pembejeo kama mbegu bora, mbolea na viuatilifu kwa ruzuku, tutaongeza upatikanaji wa maji ya uhakika na kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka ekari milioni 3.4

hadi ekari milioni tano, kwa kukamilisha ujenzi wa mabwawa na skimu za umwagiliaji zinazoendelea na kuanzisha skimu mpya ikiwemo kwenye Bonde la Mto Rufiji," alisema.

Alisema pia Benki za Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Benki ya Ushirika zitaimarishwa ili kukuza uwekezaji kwenye sekta ya kilimo, na zichochee mapinduzi yanayotazamiwa.

"Pamoja na kuongeza uzalishaji, lazima pia tudhibiti upotevu wa mazao baada ya mavuno. Hivyo, tutaendelea kuwekeza katika kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao chini ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)," alisema.

## Sekta ya Mifugo

Kuhusu sekta ya mifugo, Mhe. Rais alisema miongoni mwa ahadi za Serikali yake ni kuongeza eneo lililopimwa na kutengwa kwa shughuli za ufugaji kutoka ekari milioni 3.46 hadi ekari milioni sita.

"Hatua hii itaepusha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, na itaongeza wigo wa uzalishaji wa malisho ya mifugo ili tuelekee kwenye ufugaji wa kisasa," alisema.

Pia alisema chanjo, pamoja na utambuzi wa mifugo nchini itafanyika ili kuongeza ubora wa mazao ya mifugo, na kuweza kuingia kwenye kumbukumbu za dunia na kutambulika sokoni.

Pamoja na hatua hiyo, Mhe. Rais alisema uboreshaji utafanyika wa kosafu (sifa) za mifugo, ujenzi wa mabwawa ya kunyweshea, majosho, machinjio na miundombinu mingine muhimu kwa ajili ya ufugaji.

"Lengo ni kuwa na mnyororo wa kuongeza thamani ya mifugo na mazao ya mifugo, kwa ajili ya kuliendea soko la nje. Tutoke kwenye kumtazama ng'ombe na mlio wake, tutazame uzito wa nyama, ladha ya nyama, wingi wa maziwa, ubora wa ngozi, ubora wa kwato na pembe," alisema.

## Sekta ya Uvuvi

Kwa upande wa sekta ya uvuvi, Mhe. Rais alisema ujenzi wa Bandari ya Uvuvi iliyopo Kilwa, ambayo itazalisha fursa za ajira takribani 30,000 utakamilishwa.

Aliongeza kuwa ujenzi utafanyika wa bandari nyingine ya kisasa ya uvuvi Bagamoyo itakayofungamanishwa na kongani ya viwanda vya samaki.

"Tutafanya mapitio ya utoaji wa leseni za uvuvi kwa lengo la kuifanya nchi kufaidika ipasavyo na fursa za uvuvi wa bahari kuu," alisema.

Aidha alisema kutakuwa na uendelezaji wa utoaji wa mikopo ya boti, zana za uvuvi, makasha ya kuhifadhi samaki na miundombinu ya kukaushia.

Vilevile, alisema uwekezaji zaidi utafanyika kwenye vizimba na mabwawa ya kufugia samaki, na kuwawezesha wananchi wengi zaidi kuongeza kipato na kujikwamua kiuchumi.

"Hili litakwenda sambamba na kutafuta majawabu ya teknolojia ya chakula cha samaki ambayo imekuwa ni changamoto kubwa kwa wafugaji wa Samaki," alisema.

## Sekta ya Viwanda

Kuhusu sekta ya viwanda, Mhe. Rais alisema Serikali imejiwekea lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani kutoka asilimia 4.8 hadi kufikia asilimia tisa kwa mwaka ifikapo 2030.

Alisema safari ya muhula wa pili wa miaka mitano ya Awamu ya Sita inapoanza, malengo ni kuweka kongani za viwanda katika kila Wilaya ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi, mifugo na madini yanayozalishwa, na zitakazoweza kuzalisha bidhaa zinazohitajika kwenye masoko ya maeneo yetu.

"Tutahamasisha ujenzi wa viwanda vitakavyolisha viwanda vingine, kwa malighafi na vipuri, na viwanda vitakavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwenye masoko ya kikanda. Lengo la mkakati huu ni kuelekea kwenye Taifa linalojitegemea," alisema.

Aidha alisema ili kuitekeleza vyema ajenda ya uchumi wa viwanda, uimarishaji utafanyika wa miundombinu wezeshi ya umeme, maji, bandari, reli na barabara kwa ajili ya usafiri na usafirishaji wa malighafi na bidhaa.

## Sekta ya Madini

Kwa upande wa sekta ya madini, Mhe. Rais alisema ukamilishaji wa mkakati wa utambuzi wa madini adimu utafanyika ili Serikali itambue aina ya madini, viwango vya madini na eneo madini yalipo.

Pia alisema katika kuendeleza sekta ya madini, Serikali itapitia upya leseni zilizotolewa ili kubaini leseni ambazo hazijaendelezwa na kuchukua hatua za kuzitoa kwa wachimbaji wenye nia ya dhati ya kufanya uendelezaji wa maeneo husika.



"Wachimbaji wadogo wamekuwa nguzo ya kutegemewa katika sekta ya madini nchini. Hivyo basi, tutatenga maeneo maalum kwa ajili yao, tutawapatia leseni na tutawaendeleza kwa kuwapa mitaji na mitambo ya uchorongaji, pamoja na kuwapatia taarifa sahihi za kijiolojia," alisema.

Aliongeza kuwa katika hatua nyingine muhimu ya uongezaji wa thamani ya madini hapa hapa nchini, Serikali imedhamiria kuwa na kiwanda cha kuchenjua madini ifikapo mwaka 2030.

"Tutaondokana na kusafirisha makinikia kwenda nje ili tuokoe ajira ambazo tumekuwa tukizipoteza. Vilevile, tutaanzisha Mfuko wa Wakfu wa Madini ili fedha zitokanazo na madini zije ziwafae vizazi vijavyo. Tunafanya hivyo tukitambua kuwa madini si mahindi kwamba ukiyavuna, utatenga mbegu ili uyaoteshe tena," alisema.

"Ukichimba madini kuna mwisho wake. Tunataka vizazi vyetu visikute mashimo tu, bali wakute fedha zitokanazo na madini tunayoyavuna leo," alisema.

### Sekta ya Utalii

Kuhusu sekta ya utalii, Mhe. Rais alisema katika miaka mitano ijayo mipango ni kuendelea kuikuza zaidi sekta hiyo, lengo likiwa kufikia watalii wa ndani na nje milioni nane.

"Tunaamini kwamba, kutokana na wingi na ubora wa vivutio pamoja na utajiri mkubwa wa kitamaduni, tunaweza kufikia lengo hili. Sasa ili kukuza utalii tutafungamanisha vivutio vya utalii ili mtalii atumie siku nyingi zaidi akiwa hapa nchini," alisema.

Pia alisema jitihada za uhifadhi na utunzaji wa maliasili sambamba na kupambana na ujangili zitaendelezwa.

### Sekta ya Ujenzi

Kuhusu sekta ya ujenzi, Mhe. Rais alisema kipaumbele kitakuwa ni kukamilisha miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara ambazo tayari zimeanza na zinaendelea.

Alisema kasi itaongezwa katika utekelezaji wa miradi ya barabara kupitia TANROADS, ili tufikie lengo la kuunganisha Wilaya zote na Makao Makuu ya Mikoa kwa kiwango cha lami.

"Kwa jiji la Dar es Salaam, tutaboresha barabara kuu kwa kujenga barabara za juu katika makutano ya barabara katika maeneo ya Morocco, Mwenge, Magomeni na Tabata, na ujenzi wa awamu zilizobaki za miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (BRT)," alisema.

Alisema UDART itajengewa uwezo ili iweze kusimamia vyema uendeshaji wa mabasi ya mwendokasi.

Aliongeza kuwa bajeti na uwezo wa TARURA itaimarishwa ili kusaidia taasisi hiyo kuboresha barabara za ndani na za vijijini na kuhakikisha zinapitika mwaka mzima, na kuwa wakulima wanaweza kuyafikia masoko kwa urahisi.

"Kwa upande wa ujenzi wa makazi, jitihada zetu zitajielekeza kupunguza gharama za vifaa vya ujenzi ili tuwawezeshe wananchi kujenga makazi bora. Tutaweka mkazo maalum kwenye nyumba bora na nafuu," alisema.

Sambamba na hayo, alisema kasi itaongezwa ya urasimishaji wa maeneo ya makazi, na kuimarisha utatuzi wa migogoro ya ardhi, kwa kupima ardhi nchi nzima kwa teknolojia ya kisasa ya satelaiti.

> **Kama tutakubaliana na wawekezaji, mradi huo utabadilisha kabisa taswira na sura ya uchumi wetu. Katika majadiliano yetu tumechelewa kidogo kwa sababu tunahakikisha majadiliano hayo yanazingatia maslahi mapana ya nchi na kuhakikisha mradi huu utawanufaisha Watanzania moja kwa moja.**
>
> Rais Dkt. Samia



## Sekta ya Nishati

Kwa upande wa sekta ya nishati, Mhe. Rais alisema Serikali yake imejiwekea lengo la kuongeza uzalishaji wa umeme maradufu kufikia megawati 8,000 ifikapo mwaka 2030.

"Tutaongeza uzalishaji kwa kutumia vyanzo vya nishati mbalimbali ambazo nchi yetu imebarikiwa nazo ikiwemo maji, jua, gesi, joto ardhi na upepo, na hata umeme utokanao na nguvu ya nyuklia," alisema.

Alitaja lengo lingine kuwa ni mikoa yote ya Tanzania kuunganishwa na Gridi ya Taifa ya umeme ifikapo mwaka 2030.

Kwa upande wa gesi asilia, Mhe. Rais alisema kuna dhamira ya dhati ya kukamilisha majadiliano ya mradi mkubwa na wa kihistoria wa dola bilioni 42 wa uchimbaji wa gesi asilia.

"Kama tutakubaliana na wawekezaji, mradi huo utabadilisha kabisa taswira na sura ya uchumi wetu. Katika majadiliano yetu tumechelewa kidogo kwa sababu tunahakikisha majadiliano hayo yanazingatia maslahi mapana ya nchi na kuhakikisha mradi huu utawanufaisha Watanzania moja kwa moja," alisema.

## Reli ya Kisasa ya SGR

Kuhusu reli ya kisasa ya SGR, Mhe. Rais alisema Serikali yake itaendeleza uwekezaji kwenye ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR ya ushoroba wa kati kwa kukamilisha vipande vilivyosalia yaani Makutupora-Tabora; Tabora-Isaka; Isaka-Mwanza; na Tabora-Kigoma, na vilevile kipande kinachoenda Burundi cha Uvinza-Musongati.

"Tutakuja na mkakati wa kuhakikisha reli inatengeneza ushoroba wa uchumi, biashara na uwekezaji. Tunajipanga pia kujenga reli ya SGR kutoka Tanga hadi Musoma, na kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay (Ruvuma) inayofika pia Mchuchuma na Liganga," alisema.

Sambamba na ujenzi wa reli mpya, Mhe. Rais alisema Serikali yake itasimamia maboresho ya reli zilizopo ikiwemo reli ya TAZARA.

"Ninafurahi kuwaatarifu kuwa hivi karibuni kutafanyika hafla ya kuweka jiwe la msingi la Mradi wa Ukarabati wa Reli ya TAZARA itakayofanyika nchini Zambia," alisema.

"Aidha, kwa reli ya zamani ya Meter Gauge (MGR) tutafanya ukarabati wa vipande vya Tabora - Kigoma; Kaliua - Mpanda; Tanga - Arusha; Ruvu - Mruazi; ili nayo itumike kuchochea uchumi," alisema.

Vilevile, alisema Serikali yake inakusudia kujenga treni za kisasa katika miji ya Dar es Salaam na Dodoma ili kuboresha usafiri kwenye majiji hayo yanayokua kwa kasi kubwa sana.

## Sekta ya Uchukuzi

Kwa upande wa sekta ya uchukuzi, Mhe. Rais alisema mwelekeo wa kisera ni kujenga mfumo fungamanishi ambao utahakikisha kuwa bandari, viwanja vyote vya ndege, na vituo vya reli vina muunganiko wa usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia mbalimbali.

Alisema baada ya maboresho ya miundombinu na mifumo ya uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, gharama za uendeshaji wa bandari zimepungua ambapo zaidi ya shilingi bilioni 258 kwa mwaka zimeokolewa.

"Kuelekea mwaka 2030, tutasimamia maboresho zaidi kwenye bandari zetu nchini. Tutaongeza gati 10 kwenye Bandari ya Dar es Salaam ambayo kwa sasa ina gati 12. Tutakamilisha kuunganisha reli ya SGR na bandari ili mizigo isafirishwe kwa reli hadi Bandari Kavu ya Kwala ambapo magari ya mizigo (malori) yatafanya kazi ya usafirishaji kuanzia hapo," alisema.

Vilevile, alisema maboresho mengine yatafanyika katika bandari za Bahari ya Hindi ikiwemo Tanga, ambayo itaunganishwa kwa reli na Bandari ya Musoma iliyopo Mkoa wa Mara.

**Tutajenga pia Chuo cha Teknolojia ya Kidijitali ili kuwajengea vijana wetu uwezo wa kushindana katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia,**

Rais Dkt Samia Suluhu Hassan

"Tutafanya upanuzi na maboresho kwenye bandari ya Mtwara ambayo nayo, tunakusudia kuiunganisha kwa reli na bandari inayojengwa Mbambabay kule Nyasa, Ruvuma," alisema.

Alisema pia bandari za maziwa makuu za Mwanza, Kigoma na Kalema kule Tanganyika zitaboreshwa pamoja na kukamilisha ukarabati na ujenzi wa meli za abiria na mizigo zitakazotoa huduma kupitia bandari hizo.

Kwa upande wa usafiri wa anga, Mhe. Rais alisema mipango ni kuliimarisha zaidi Shirika la Ndege la Tanzania kwa kuongeza ndege mpya nane ili kuliwezesha shirika kuongeza miruko ndani na nje ya nchi.

"Tumepanga kuwa ifikapo mwaka 2030 mwelekeo wetu ni kufungua nchi pamoja na kukifanya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere kuwa kiungo cha safari za ndege kimataifa," alisema.

Alisema pia ukamilishwaji utafanyika wa ujenzi wa viwanja mbalimbali unaoendelea, vikiwemo Kiwanja cha Kimataifa cha Msalato - Dodoma, na viwanja vya Mwanza, Iringa na Mpanda.

## Sekta ya TEHAMA

Kuhusu sekta ya TEHAMA, Mhe. Rais alisema Serikali itahakikisha huduma ya mtandao inawafikia Watanzania wengi zaidi ili iwasaidie kujiunga katika mifumo ya upatikanaji wa fedha na kukuza biashara zao kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na kampuni za watoa huduma.

"Tutajenga pia Chuo cha Teknolojia ya Kidijitali ili kuwajengea vijana wetu uwezo wa kushindana katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia," alisema.

Kuhusu vyombo vya habari, Mhe. Rais alisema Serikali yake itaendelea kutoa leseni kwa vyombo vya habari, na kulinda uhuru wa kufanya kazi zao, kwa kufuata sheria za nchi.

"Tutaimarisha Vitengo vya Habari vya Serikali ili viweze kutoa habari kwa weledi na kwa wakati. Aidha, tutaendelea kutambua waandishi wa habari za maendeleo nchini kupitia Tuzo ya Samia Kalamu Awards," alisema.



# Mhe. Mussa Azzan Zungu achaguliwa kuwa Spika wa Bunge la 13

**Aweka historia ya kupata kura nyingi za wabunge**

*Na. Deonisius Simba*

**Mbunge wa Jimbo la Ilala (CCM), Mhe. Mussa Azzan Zungu amechaguliwa kuwa Spika wa Bunge la 13 na kuweka historia ya kupata kura nyingi za Wabunge.**

Kabla ya kushika nafasi hiyo Mhe. Zungu alikuwa Naibu Spika katika Bunge la 12 ambalo Spika wake alikuwa Mbunge wa Uyole, Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb) ambaye kwenye kinyang'anyiro hicho aliamua kujitoa katika hatua za awali.

Katika uchaguzi huo uliofanyika Novemba 11, 2025, ulihusisha wagombea sita ambapo Mhe. Zungu aliibuka mshindi kwa kupata kura 378 huku washindani wake watano wakigawana kura mbili huku kura tatu zikiharibika katika kura 383 zilizopigwa.

Msimamizi wa uchaguzi huo ambaye pia ni Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard alimtangaza Mhe. Zungu katika matokeo yaliyokuwa na ushindani wa wagombea sita.

"Kwa matokeo haya, naomba kumtangaza Mhe. Mussa Azzan Zungu kuwa amechaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla ya kura 378, matokeo hayo yamethibitishwa kwa kusainiwa na wagombea na wasimamizi wao," alisema Baraka Leonard.

Uchaguzi huo ulifanyika katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge la 13 kilichoongozwa na Mbunge wa Isimani, Mhe. William Lukuvi, Mhe. Zungu alifanikiwa kuwashinda washindani wenzake watano ambao watatu kati yao walipata kura sifuri

Waliogombea wengine walikuwa ni Chrisant Ndege kutoka DP, Veronica Charles wa NRA na Amin Alfred wa ADC, ambao kila mmoja alipata kura sifuri na walikubali matokeo hayo.

Wengine waliokuwepo kwenye ushindani huo ni Anitha Khalfan Mgaya wa NLD na Ndonge Said Ndonge wa AAFP walipata kura moja kila mmoja, huku kura tatu zikiharibika.



Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azzan Zungu aliwashukuru Wabunge wote wateule kwa kuonesha imani na kumchagua kwa kura nyingi.

Mhe. Zungu alisema ushindi wake ni ushindi wa Bunge na Wabunge wote kwani anaamini katika haki na uwazi.

"Nitatoa ushirikiano kwa viongozi wenzangu watakaochaguliwa akiwemo Naibu Spika na Wenyeviti, mimi nilipewa ushirikiano na Mhe.Dkt. Tulia Ackson, alinipa uhuru wa kujifunza mambo mengi nami nitafanya hivyo," alisema Mhe. Zungu.

"Nitatoa fursa sawa kwa Waheshimiwa Wabunge wote, na kwamba ofisi ya Spika itakuwa wazi kwa kila Mbunge kwa ushauri mbalimbali, asanteni sana Waheshimiwa naomba muondoe mashaka," aliongeza.

Hii ni mara ya nne mfululizo kwa Naibu Spika kuchaguliwa kuwa Spika. Aliyekuwa Naibu Spika katika Bunge la Tisa Mhe. Anne Makinda alichaguliwa kuwa Spika katika Bunge la 10.

Hayati Job Ndugai alikuwa Spika wa Bunge la 11 akipanda kutoka Naibu Spika wa Bunge la 10 kama ilivyokuwa kwa Dkt. Tulia Ackson ambaye alikuwa Naibu Spika lakini Bunge la 12 akawa Spika.

Mhe. Zungu amekuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka 20 huku akiingia Bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 2005.



> **Uwezo na uzoefu alionao Mhe. Zungu hautiliwi shaka katika utumishi wake ndiyo maana hakuona shida kuchaguliwa kwake.**

**Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Cecilia Paresso**

Nafasi zingine alizowahi kushika mbali na Naibu Spika, amewahi kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mwenyekiti wa Bunge (2012-2021), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, na amefanya kazi na Maspika wanne wa Mabunge hayo, akiwemo Hayati Samuel Sitta Mhe. Anne Makinda, Hayati Mhe. Job Ndugai na Mhe. Dkt. Tulia Ackson.

Waheshimiwa Wabunge wamepokea kwa furaha ushindi wake wakieleza kuwa Mhe. Zungu ni mtu wa kuwaunganisha watu, kazi aliyoiweza akiwa Naibu Spika, hivyo wanaamini ataweza zaidi akiwa Spika.

Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Cecilia Paresso alisema uwezo na uzoefu alionao Mhe. Zungu hautiliwi shaka katika utumishi wake ndiyo maana hakuona shida kuchaguliwa kwake.

Naye Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Mhe. Ado Shaibu alipongeza kuchaguliwa kwa Mhe. Zungu ambako alisema licha ya kuwa yeye anatoka kundi la Wabunge Walio Wachache Bungeni lakini anaamini watapewa nafasi na sauti zao kusikika chini ya uongozi wa Mhe. Zungu.



# Dkt. Mwigulu Nchemba ateuliwa kuwa Waziri Mkuu

*Na. Halima Laizer*

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amemteua Dkt. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuthibitishwa na Bunge.**

Baada ya uteuzi wa Waziri Mkuu, Rais alituma jina hilo Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Wabunge, shughuli iliyofanyika tarehe 13 Novemba, 2025 katika Kikao cha Tatu cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge la 13.

Dkt. Nchemba ambae pia ni Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi aliwahi kuwa Waziri wa Fedha katika Serikali iliyopita.

**“Dkt. Nchemba anajulikana kama mfano wa mafanikio yanayotokana na bidii na kujituma na kwamba alikulia katika mazingira ya kijijini na alitoka katika familia yenye hali ya kawaida ambapo aliwahi kuchunga ng’ombe nyikani akiwa kijana mdogo”**

*Spika wa Bunge,* ***Mhe. Mussa Zungu***

Kufuatia kuwasilishwa kwa jina hilo Bungeni na kutangazwa na Spika wa Bunge, Mhe. Mussa Zungu, Wabunge walipiga kura kwa ajili ya kuthibitisha jina hilo la Waziri Mkuu.

Akitangaza matokeo ya kura, Spika wa Bunge, Mhe. Zungu alisema Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba amethibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura 369 kati ya kura 371 zilizopigwa.

Awali akiwasilisha Hoja ya Serikali kuliomba Bunge la kumthibitisha Waziri Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe.Hamza Johari alisema Azimio hilo linawasilishwa Bungeni kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

“Bunge linaazimia kwamba Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la Uchaguzi la Iramba Magharibi na ambaye ameteuliwa na Rais kuwa Waziri Mkuu, amethibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa 11 kwa mujibu wa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

“Majukumu makubwa ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ninaliomba Bunge lako lithibitishe uteuzi wake yameainishwa katika Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema Waziri Mkuu atakuwa na madaraka ya juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

“Waziri Mkuu atakuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Katika utekelezaji wa madaraka yake, Waziri Mkuu atatekeleza au kusababisha utekelezaji wa jambo lolote au mambo yoyote ambayo Rais ataagiza kwamba yatekelezwe”

“Kwa kifupi Waziri Mkuu ni kiungo muhimu kati ya Bunge na Serikali. Kwa maneno mengine yeye ni daraja muhimu kati ya wananchi na Serikali na ni msaidizi mkuu wa Rais katika kutekeleza majukumu yake,” alisema.

Alisema Dkt. Nchemba anajulikana kama mfano wa mafanikio yanayotokana na bidii na kujituma na kwamba alikulia katika mazingira ya kijijini na alitoka katika familia yenye hali ya kawaida ambapo aliwahi kuchunga ng’ombe nyikani akiwa kijana mdogo.

“Maisha hayo yalimfundisha nidhamu, uvumilivu na kuthamini kazi halali. Mara kadhaa amekuwa akisimulia hadithi ya maisha yake kama njia ya kuwahamasisha vijana kupambana kupitia elimu na kujituma,” alisema.

Wakichangia hoja kabla ya kupiga kura ya kumthibitisha, baadhi ya Wabunge waliopata fursa ya kuzungumza walipongeza uteuzi wa Dkt. Nchemba kutokana na uchapakazi wake na tabia yake ya kujishusha.

Mbunge wa Jimbo la Ismani, Mhe. William Lukuvi, alisema, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ni mchumi mbobevu aliyesimamia makusanyo ya kodi na kuisaidia Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kutekeleza vyema miradi ya maendeleo.

Alisema kwa kazi nzuri iliyofanywa na utawala wa Rais Samia akisaidiwa na Dkt. Nchemba, imewezesha pia Wabunge wengi wa CCM kuaminiwa na kurejea tena Bungeni.

Alisema Dkt. Samia Suluhu Hassan hajakosea kumteua Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania kutokana na weledi, uwezo na uzoefu wake katika uongozi nchini.

Mbunge wa Peramiho, Mhe. Jenista Mhagama, alisema Waziri Mkuu mpya, Dkt. Mwigulu Nchemba, ni mtu mwenye maono ya kujua taifa linataka kwenda wapi.

Alisema Dkt. Nchemba atakuwa ni Waziri Mkuu anayelitazama taifa kwa miaka 25 mbele, kutokana na kuwa ni miongoni mwa mawaziri walioshiriki katika kuandaa Dira 2050, hivyo utekelezaji wa maono ya Rais Samia Suluhu Hassan unahitaji mtu wa aina yake.

“Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita yasingepatikana kama kusingekuwa na Waziri



wa Fedha ambaye angetekeleza majukumu yake, na pia ni miongoni mwa mawaziri ambao wametengeneza Dira ya Taifa ambayo tutakwenda nayo hadi 2050," alisema.

Alisisitiza kuwa Dkt. Nchemba pia alikuwa ni miongoni wa wajumbe walioandaa Ilani ya Uchaguzi 2025/2030, hivyo anaifahamu ilani hiyo na atakwenda kuisimamia vizuri.

Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, Mhe. Anne Kilango Malecela, alisema Waziri Mkuu Mteule, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ni kiongozi wa watu anayefikiwa na kila mtu.

**Katika historia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uteuzi na uthibitisho wa Waziri Mkuu ni hatua ya msingi katika kuimarisha utawala wa Taifa na kutekeleza Sera za Serikali kwa ufanisi.**



Alisema katika nafasi zake alizowahi kushika kuanzia Naibu Waziri wa Fedha na Waziri wa Fedha tofauti na mawaziri wengine amekuwa msikivu anayesikiliza watu na kwamba Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amegusa mioyo ya wengi kwa kumteua.

Kwa upande wake, Mbunge wa Kibakwe, Mhe. George Simbachawene, alimmwagia sifa Waziri Mkuu mpya, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kuwa ni mbobevu kwenye uongozi.

Aidha, alisema umri wake wa miaka 50 unaweza kubeba kila rika la anaowaongoza hasa kundi la vijana wengi ambao ni Wabunge waliopo Bungeni.

## Historia ya Dkt. Nchemba

Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba alizaliwa tarehe 7 Januari, 1975 katika Kijiji cha Makunda, Wilaya ya Iramba, Mkoani Singida.

Alisoma Shule ya Msingi Makunda mkoani Singida kati ya mwaka 1987 hadi 1993, kisha akaendelea na masomo ya Sekondari katika Shule ya sekondari Ilboru mkoani Arusha na Sekondari ya Mazengo mkoani Dodoma ngazi ya kidato cha tano na sita.

Baada ya hapo alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambako alisomea Shahada ya Kwanza ya Uchumi na baadaye akahitimu Shahada ya Uzamili mwaka 2006, na baadaye kupata Shahada ya Uzamivu kutoka chuo hicho hicho.

Safari yake ya kisiasa ilianza kupanda kasi mwaka 2010 aliposhinda Ubunge wa Jimbo la Iramba Magharibi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alirudi tena bungeni mwaka 2015 huku ndani ya chama chake akijipatia heshima kama kiongozi mwenye msimamo thabiti na anayejali nidhamu katika utumishi wa umma.

Amewahi kuwa Katibu Mkuu Msaidizi, Mjumbe wa Kamati Kuu, Halmashauri Kuu na Sekretarieti ya Chama kwa miaka mingi.

Dkt. Nchemba amewahi kushika nafasi mbalimbali serikalini ambapo alianza kama Naibu Waziri wa Fedha katika Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Rais Dkt. Jakaya Kikwete.

Baadaye aliteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi mwaka 2015, kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mwaka 2016.

Mwaka 2021 aliteuliwa kuwa Waziri wa Fedha, nafasi aliyoishikilia hadi uteuzi wake kuwa Waziri Mkuu.

Mhe. Dkt. Nchemba anakuwa Waziri Mkuu wa Kumi na Moja wa Tanzania, akifuata nyayo za Mawaziri Wakuu wengine.

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ndiye aliyekuwa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Serikali ya Tanganyika Huru kuanzia Desemba, 1961 hadi Januari, 1962 alipojiuzulu.

Akizungumza mara baada ya kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Nchemba, aliahidi kuwatumikia wananchi na kwamba yeye hajausoma umaskini kwenye vitabu bali anaujua na ameuishi kwa takribani miaka thelathini na mbili.

"Natambua hali ya umaskini uliopo nchini kwa sababu nimeishi na hali hiyo kwa zaidi ya miaka thelathini na mbili, natambua changamoto ya ajira kwa vijana nchini, natambua ugumu wa maisha uliopo." Alisema

Aidha, aliwaonya watumishi wa umma wazembe, wala rushwa pamoja na wale wenye lugha chafu kuwa wanapaswa kujirekebisha kwa kuwa hawatakuwa na nafasi.

Katika historia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uteuzi na uthibitisho wa Waziri Mkuu ni hatua ya msingi katika kuimarisha utawala wa Taifa na kutekeleza Sera za Serikali kwa ufanisi.

“

**Kifungu cha 51(1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977,**

Kinampa mamlaka Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteua Waziri Mkuu kutoka miongoni mwa Wabunge. ”

Kifungu cha 51(1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kinampa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteua Waziri Mkuu kutoka miongoni mwa Wabunge.

Aidha, kifungu cha 51(2) kinatoa msingi wa uteuzi wa Waziri Mkuu, kwamba Rais atamteua Mbunge wa kuchaguliwa katika Jimbo la Uchaguzi kuwa Waziri Mkuu baada ya kushika madaraka yake ndani ya siku kumi na nne.

Kifungu hicho kinaeleza kwamba Waziri Mkuu huyo atateuliwa kutoka chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi Bungeni au kama hakuna chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi yule anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge walio wengi.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa Azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi.



# Bunge la 13 laanza, Wabunge waapishwa.

*Na. Deborah Sanja*

**Mkutano wa Kwanza wa Bunge la 13 ulianza rasmi kikao chake cha kwanza Novemba 11, 2025 kufuatia Tangazo la Rais la kuitisha Bunge lililotolewa katika Gazeti la Serikali.**

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Mwaka 1977, Rais ndiye aliyepewa mamlaka ya kuliitisha Bunge baada ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu.

Kufuatia Tangazo hilo, Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard alitoa tangazo la kuwaita Wabunge Wateule Jijini Dodoma Novemba 8, 2025 kwa ajili ya shughuli za usajili na taratibu nyingine za kiutawala kabla ya kuanza kwa Kikao cha Kwanza.

Wabunge Wateule walitakiwa kufika na nyaraka mbalimbali kwa ajili ya usajili ikiwemo Hati ya Kuchaguliwa/Kuteuliwa kwa Mbunge, Kitambulisho cha Taifa, Kadi ya Benki, Cheti cha Ndoa kinachotambuliwa na Serikali (kwa wenye ndoa), vyeti vya kuzaliwa vya watoto wenye umri chini ya miaka 21 (kwa wenye watoto/wasiozidi wanne) na Vyeti vya Elimu/Taaluma

Baada ya siku tatu za usajili, Kikao cha Kwanza kilianza ambapo shughuli ya kwanza iliyofanyika













**"Bunge ni chombo cha kuisimamia Serikali ikiwemo kutunga sheria hivyo ni matarajio yake kwamba Bunge la 13 litatekeleza wajibu wake huo wa kikatiba na kisheria,".**

*Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini* **Mhe. Ado Shaibu**

ni uchaguzi wa Spika wa Bunge ambaye baada ya kuchaguliwa na kuapishwa alianza kuwaapisha Wabunge.

Shughuli hiyo ya kuwaapisha Waheshimiwa Wabunge Wateule ilifanyika kwa kwa siku mbili ambapo Wabunge takribani 391 waliapishwa na Mheshimiwa Spika.

Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakizungumza baada ya kuapishwa walisema Bunge la 13 litafanya kazi yake ipasavyo ya kuwahudumia Watanzania.

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mhe. Mwita Waitara akizungumzia Bunge hilo jipya alisema ni muhimu Bunge likajipanga kuhudumia wananchi chini ya uongozi wa Spika wa Bunge, Mhe. Mussa Azzan Zungu.

"Wananchi wawe na matumaini makubwa na Bunge hili, wawe na matumaini na Waheshimiwa Wabunge kwamba tutafanya mambo makubwa zaidi, na mimi ni miongoni mwa Wabunge ambao tumejipanga kutokupoa kabisa, nimewaahidi wananchi wangu pale nilipoishia nitaanzia pale na ikiwezekana nitazidisha zaidi kwenda mbele," alisema.

**"Bunge la 13 litakuwa ni Bunge la kisasa linalochapa kazi ili kuhakikisha wananchi wanatetewa na kwamba wapo tayari kujenga hoja na kutetea zile zitakazoletwa ndani ya Bunge ikiwemo zile za mbunge mmojammoja,".**

*Mbunge wa Jimbo la Shaurimoyo Mhe.Mattar Salum Ali*


Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini Mhe. Ado Shaibu akizungumza baada kuapishwa alisema Bunge ni chombo cha kuisimamia Serikali ikiwemo kutunga sheria hivyo ni matarajio yake kwamba Bunge la 13 litatekeleza wajibu wake huo wa kikatiba na kisheria.

Alisema yeye akishirikiana na Wabunge wote bila kujali vyama wanavyotoka watahakikisha wanautekeleza wajibu huo vizuri kwa maslahi ya wananchi.

Mbunge wa Jimbo la Shaurimoyo Mhe. Mattar Salum Ali alisema anaamini Bunge la 13 litakuwa ni Bunge la kisasa linalochapa kazi ili kuhakikisha wananchi wanatetewa na kwamba wapo tayari kujenga hoja na kutetea zile zitakazoletwa ndani ya Bunge ikiwemo zile za Mbunge mmoja mmoja.

Kwa upande wake Mbunge wa Kyela, Mhe. Baraka Mwamengo, aliwashukuru wananchi wa Kyela kwa kumuamini na kumpa dhamana hiyo.

Alimpongeza Mhe. Rais na Serikali yake kwa kazi kubwa iliyofanywa katika Jimbo hilo na kusema kazi ya Wabunge itakuwa ni kushinikiza fedha za maendeleo zinazotolewa katika majimbo na kuhakikisha zinatumika vizuri katika malengo yaliyokusuduwa.




# Mhe. Daniel Sillo achaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la 13

## Ni baada ya Kupata Ushindi wa Asilimia Mia Moja wa kura 371 za Waheshimiwa Wabunge

*Na. Christina Nkya*

**Mbunge wa Babati Vjijini, Mhe. Daniel Baran Sillo amechaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Kikao cha Tatu cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge la 13 kilichofanyika Novemba 13, 2025.**

**Mhe. Sillo ambaye alikuwa mgombea pekee katika nafasi hiyo alipata ushindi wa asilimia mia moja baada ya kupata kura za ndio 371 za Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwepo bungeni wakati uchaguzi unafanyika.**

**Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Mhe. Sillo aliwashukuru Wabunge kwa imani kubwa waliyomuonesha na kuahidi ushirikiano.**

**Aidha aliwaomba pia Wabunge wampe ushirikiano ili aweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.**

"Ninyi Wabunge wenzangu naomba ushirikiano wenu katika kutimiza majukumu ambayo nimekabidhiwa siku hii ya leo," alisema.

Mhe. Sillo alimshukuru pia Spika wa Bunge na kuahidi kumpa ushirikiano katika kutimiza majukumu yake kwa manufaa ya Watanzania wote.

"Binafsi nikushuru wewe Mheshimiwa Spika na niahidi kukupa ushirikiano mkubwa na kukushauri kwa uadilifu mkubwa katika kutimiza majukumu yote yaliyopo mbele yetu kwa manufaa ya Watanzania," alisema.

## Historia ya Mhe. Daniel Sillo

Mhe. Daniel Sillo alizaliwa mwaka 1972 Wilayani Babati, Mkoa wa Manyara na mwaka 1992 alihitimu elimu ya kidato cha nne katika shule ya Sekondari ya Tanga pia mwaka 1995 alihitimu kidato cha sita katika Shule ya Sekondari ya Moshi.

Aidha mwaka 1999 alitunukiwa Stashahada ya Juu ya Uhasibu kutoka katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM). Vilevile mwaka 2003 alitunukiwa Stashahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Kodi kutoka katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM). Pamoja na hayo, mwaka 2011 alitunukiwa Shahada ya Uzamili ya Biashara kutoka katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## Safari ya Kisiasa

Safari ya kisiasa ya Mhe. Sillo ilianza mwaka 2015, alipojitosa kwa mara ya kwanza kuwania Ubunge, ingawa hakufanikiwa. Hata hivyo, hakurudi nyuma ambapo mwaka 2020 alirejea tena kwa nguvu mpya na kuibuka na ushindi, hatua iliyompa nafasi ya kuwa mwakilishi wa wananchi wa Babati Vijijini.

Mara baada ya kuingia bungeni, Mhe. Sillo alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na baadaye Mwenyekiti wa Bunge.

Safari ya Mhe. Sillo katika Bunge la 12 haikuishia hapo kwani mwaka 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kabla ya kuingia katika siasa Mhe. Daniel Sillo alikuwa mtumishi wa umma katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) .

## Walioshika wadhifa wa Naibu Spika


Mbali na Mhe. Sillo wengine waliohudumu katika nafasi ya Naibu Spika baada ya uhuru ni pamoja



na Mhe. Erasto Mbwana Mang'enya aliyehudumu mwaka 1960 hadi 1961, akapata nafasi tena mwaka 1966 hadi 1973, Mhe. Frank Mfundo mwaka 1962 hadi 1964, Mhe. Herman E. Sarwatt mwaka 1964 hadi 1965, Mhe. Stanslaus Kasusura mwaka 1973 hadi 1985, Mhe. Austin K. Shaba mwaka 1986 hadi 1988 na Mhe. George M. Nhigula mwaka 1988 hadi 1990.

Wengine ni Mhe. Pius Msekwa mwaka 1990 hadi 1994, Mhe. Mathias Kihaule mwaka 1994 hadi 1995, Mhe. Phillip Marmo mwaka 1995 hadi 2000, Hayati Mhe. Juma J. Akukweti mwaka 2000 hadi 2005, Mhe. Anne S. Makinda mwaka 2005 hadi 2010, Hayati Job Y. Ndugai mwaka 2010 hadi 2015, Mhe. Dkt. Tulia Ackson 2015 hadi 2022 na Mhe. Mussa A. Zungu mwaka 2022 hadi 2025.

# Usimamizi wa Kibunge wa Fedha za Umma




*Na. Athuman Hussein, ndc*

a.brambati@Bunge.go.tz

**Safu hii ya usimamizi wa kibunge wa fedha za umma inaendelea kujikita katika mchakato wa kikatiba na kisheria unaofanywa na Bunge. Lengo la mchakato huo ni kuhakikisha kuwa fedha za umma zinakusanywa inavyostahili, zinatumika inavyopaswa na matumizi yake yanasimamiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu stahiki.**

Katika toleo la kumi, ufafanuzi ulitolewa kuhusu aina ya usimamizi wa fedha za umma baada ya matumizi (ex – post financial oversight), lakini ufafanuzi huo ulikuwa ni mwendelezo wa toleo la tisa lililoelezea usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kabla ya matumizi (Ex – ante financial oversight).

Kwa madhumuni ya kujenga msingi wa kubeba mwendelezo, inapendeza kuanza kwa kufafanua na kutofautisha aina hizo mbili za usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma. Aina iliyodadavuliwa katika toleo la tisa inajulikana kuwa ni "Usimamizi wa Kibunge wa Matumizi ya Fedha za Umma Kabla ya Matumizi". Aina hii ya usimamizi wa kibunge inahusisha hatua za Bunge kuweka



**Kwa ufafanuzi rahisi wa dhana hiyo, kuna umuhimu wa kurejea maana ya neno "uwajibikaji".**

Kamusi Kuu ya Kiswahili, Toleo la 3, katika ukurasa wa 1111 imefafanua kuwa uwajibikaji ni kutekeleza jukumu kwa uaminifu. Kwa mujibu wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), katika ukurasa wa 710 wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la Mwaka 2019, uwajibikaji ni hali ya kuwajibika. Kwa maneno mengine, uwajibikaji ni hali ya kukosa hiari katika kufanya jambo.

misingi ambayo inatumika kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Hatua hizo ni pamoja na upitishaji wa bajeti *(budget approval),* uidhinishaji bajeti kisheria *(budget appropriation)* na ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti *(budget oversight).*

Lengo katika usimamizi huo ni kuhakikisha kuwa kuna mipango mizuri ya matumizi ya fedha za umma, mgawanyo unaofaa wa fedha za umma kabla ya matumizi na uidhinishaji wa fedha za matumizi unaozingatia maslahi ya wananchi. Kwa upande mwingine, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma baada ya kufanyika kwa matumizi *(ex – post financial oversight)* ni mapitio ya Bunge katika kutathmini matumizi ya fedha za umma kwa kutumia hesabu za fedha. Lengo lake hasa ni kujiridhisha iwapo fedha za umma zimetumika kwa mujibu wa sheria, kwa ufanisi na kwa makusudio yake.

Aina hizo mbili za usimamizi wa matumizi ya fedha za umma zinahusiana na kukamilisha dhima ya Bunge katika eneo la fedha za umma. Aina ya usimamizi kabla ya matumizi *(Ex – ante financial oversight)* inaweka misingi ya kuzuia matumizi mabaya ya fedha za umma. Aina ya pili ambayo ni usimamizi wa fedha za umma baada ya matumizi yake *(Ex – post financial oversight)* inabeba dhana ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma (*The concept of accountability in public expenditure).* Aina zote mbili zinaimarisha nidhamu ya kibajeti (*Fiscal discipline*), uwazi katika matumizi ya rasilimali za umma na misingi ya utawala bora katika usimamizi wa fedha za umma.

Kwa msingi huo, toleo la kumi lilimalizia kwa dhana ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ikinasibishwa na msingi wa utawala bora na maendeleo ya kweli ya taifa. Umaliziaji huo unaarifu kuwa toleo hili linatakiwa kuendeleza dhana ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Kwa ufafanuzi rahisi wa dhana hiyo, kuna umuhimu wa kurejea maana ya neno "uwajibikaji". Kamusi Kuu ya Kiswahili, Toleo la 3, katika ukurasa wa 1111 imefafanua kuwa uwajibikaji ni kutekeleza jukumu kwa uaminifu. Kwa mujibu wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), katika ukurasa wa 710 wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la Mwaka 2019, uwajibikaji ni hali ya kuwajibika. Kwa maneno mengine, uwajibikaji ni hali ya kukosa hiari katika kufanya jambo.

Aidha, uwajibikaji ni dhamana ya usimamiaji wa kazi kama ilivyobainishwa katika ukurasa wa 254 wa Kamusi ya Visawe iliyoandaliwa na Profesa Mohamed A. Mohamed kwa pamoja na Profesa Said A. Mohamed, wote wazaliwa wa Unguja. Hii inaweza kumaanisha kuwa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ni dhamana ya kazi ya kusimamia matumizi ya fedha za umma.

Kutokana na ufafanuzi huo, sasa ni rahisi kuona kuwa dhana ya "uwajibikaji wa kibunge katika matumizi ya fedha za umma" inahusisha majukumu ya Bunge lenye madaraka kwa niaba ya wananchi na Serikali yenye mamlaka ya kiutendaji kutumia fedha za umma. Kwa fasili yenye wepesi kueleweka (*simple definition*), uwajibikaji wa kibunge ni hali ya Serikali kuwa na dhamana ya kusimamia matumizi ya fedha za umma na kulazimika kueleza sababu za matumizi na hatua zake kutokana na matoeko ya matumizi ikishawishi misingi ya hatua hizo.

Katika uga wa matumizi ya fedha za umma, uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ni wajibu wa maofisa wa serikali na taasisi za umma kusimamia na kutumia fedha za umma kwa namna ya kuwajibika, uwazi na ufanisi kwa kuzingatia sheria na madhumuni yaliyokusudiwa. Fasili hii imebeba mambo makuu manne ambayo ni wajibu, madhumuni yaliyokusudiwa, uwazi na ufanisi. Ufuatiliaji na mijadala katika mchakato wa usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma, hulenga kujiridhisha iwapo mambo hayo yamezingatiwa.

Kwa maana hiyo, usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma unahusiana kwa karibu na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Uhusiano uliopo kati ya dhana hizo mbili ni wa kutegemeana ambapo, kimoja hakiwezi kuwepo kwa ufanisi bila kingine.

Kwa kuwa safu hii inahusu usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma, inafaa kudadavua namna uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma unavyohusiana na usimamizi wa Kibunge wa Matumizi ya Fedha za Umma. Kimaudhui usimamizi wa kibunge ni mchakato wa Bunge kufuatilia, kuchambua na kutathmini hatua na matumizi ya Serikali.

Kwa upande mwingine, uwajibikaji wa matumizi ya fedha za umma si mchakato wa kibunge bali ni hali au utaratibu wa viongozi wa Serikali na taasisi za umma kuwajibika katika kupanga na kufanya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na madhumuni ya matumizi.

Uhusiano kati ya usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma kama ilivyoelezwa awali, ni wa kutegemeana na kuimarishana. Namna nne zinaweza kueleza kutegemeana na kuimarishana kwa dhana hizo mbili.

**Kwanza**, ni kazi za dhana hizo. Kazi ya usimamizi wa kibunge wa fedha za umma ni kufuatilia na kuchambua hatua za kifedha za serikali katika matumizi. Kazi ya uwajibikaji katika matumizi ya



> "Matokeo ya kazi za Kamati za Bunge Zinazosimamia Matumizi ya Fedha za Umma yanawezesha Serikali na maofisa wanaohusika kuchukua hatua za marekebisho. Hatua hizo ni kama vile kurejesha fedha au hatua za kinidhamu inapobidi."
>
> Jambo la Tatu linahusu hatua stahiki

fedha za umma ni kuhakikisha kuwa kuna matumizi makinifu, ya msingi na yenye uwazi. Kwa namna hiyo, usimamizi wa kibunge unalazimisha uwajibikaji kwa kufichua dosari au matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Pili**, ni lengo la kila dhana. Lengo la usimamizi wa kibunge ni kudhibiti na kusimamia matumizi ya fedha za umma. Kwa upande mwingine, lengo la Uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ni kukuza ufanisi na uadilifu kwenye matumizi ya fedha za umma serikalini. Kwa namna hiyo, vyote vinalenga kulinda fedha za umma na kujenga imani ya wananchi.

**Tatu,** ni mchakato. Usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma unahusisha kuidhinisha matumizi, kuandaliwa kwa ripoti za matumizi, ukaguzi wa ripoti za fedha, uchambuzi wa kibunge wa ripoti za ukaguzi na mahojiano kati ya Kamati za Bunge na Maofisa wa Serikali. Kwa upande mwingine, uwajibikaji unahusika kupanga kwa umakini matumizi, kuchukua hatua stahiki kadiri ya uamuzi wa Bunge, kutoa maelezo kuhusu hatua za matumizi ya fedha za umma au matokeo yake na kuchukua hatua sahihi kulingana na matokeo ya mchakato wa usimamizi wa kibunge. Ufafanuzi huo wa michakato, unadhihirisha kwamba, uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma huimarika pale ambapo kuna usimamizi madhubuti wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma.

**Nne,** ni matokeo ya kazi za dhana hizo mbili. Matokeo ya usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma ni uamuzi bora na mageuzi ya kisera kwenye uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Kwa upande mwingine, matokeo ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ni nidhamu ya kifedha na kupungua kwa ufisadi. Hali hiyo, inaarifu kuwa usimamizi wa kibunge ulio madhubuti huzaa uwajibikaji thabiti katika matumizi ya fedha za umma.

Kwa maelezo hayo, bila usimamizi wa kibunge, uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma utalegalega. Aidha, usipokuwepo uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma, usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma na ukaguzi wa ripoti za matumizi ya fedha za umma, vitakosa mantiki.

Kwa muktadha huo, Kamati za Bunge za Kusimamia Matumizi ya Fedha za Umma zinapochambua ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinahoji kuhusu matumizi ili kupata maelezo. Katika kufanya hivyo kuna mambo matatu yanachomoza.

**Jambo la kwanza** linahusu dhima ya mchakato wa usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma. Mchakato huo hufichua dosari za kiusimamizi na utekelezaji. Hivyo, hubainisha matumizi mabaya ya fedha za umma kutokana na dosari hizo.

**Jambo la pili**, ni kuhusu wajibu wa maafisa wanaohusika na matumizi ya fedha za umma. Mchakato wa Kamati za Bunge husababisha maofisa wanaohusika na matumizi ya fedha za umma kulazimika kutoa maelezo na kuwajibika.

**Jambo la tatu** linahusu hatua stahiki. Matokeo ya kazi za Kamati za Bunge Zinazosimamia Matumizi ya Fedha za Umma yanawezesha Serikali na maofisa wanaohusika kuchukua hatua za marekebisho. Hatua hizo ni kama vile kurejesha fedha au hatua za kinidhamu inapobidi.

Mambo hayo matatu, yanasisitiza kuwa usimamizi wa kibunge (*parliamentary oversight*) hutoa njia na nyenzo za uwajibikaji, ilhali uwajibikaji huhakikisha uadilifu, ufanisi na uwazi katika matumizi ya fedha za umma. Hali hiyo inachangia kuimarisha utawala bora katika matumizi ya fedha za umma.

Kwa msingi huo, umuhimu wa usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma hauishii katika kutambua kasoro au kuwawajibisha watendaji pekee, bali unaenda mbali zaidi kwa kujenga utamaduni wa uwajibikaji wa kudumu katika sekta ya umma. Kupitia kazi za Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma, Bunge hufanikisha utekelezaji wa misingi ya uwazi, nidhamu ya kifedha na matumizi sahihi ya rasilimali, huku likiwa kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi katika kuhakikisha fedha za umma zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Hatimaye, usimamizi huu wa kibunge huimarisha imani ya wananchi kwa taasisi za umma, huku ukichochea uwajibikaji wa kitaasisi na kuendeleza misingi ya utawala bora, demokrasia na maendeleo endelevu ya taifa.

Katika toleo hili, makala imerejea toleo la kumi ili kuonesha muumano wa kimaudhui na toleo hili. Kwa muhtasari, toleo hili limefafanua dhana ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma na uhusiano baina yake na dhana ya usimamizi wa kibunge wa fedha za umma. Aidha, ufafanuzi umebainisha kuwa, uhusiano kati ya usimamizi wa kibunge na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ni wa kutegemeana na kukamilishana.

Fauka ya hayo, tofauti kati ya dhana hizo imeelezwa na lengo lao la jumla limewekwa bayana. Katika toleo lijalo ufafanuzi utaendelezwa zaidi ikiwemo kueleza jinsi Bunge linavyowezesha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Muhimu kukumbuka ni busara ya waungwana kwamba, "mbegu nzuri huota mvua ya pili". Hima kwa wasomaji wa safu hii, kutolikosa toleo lijalo.

## Tuwakumbuke!



Rais wa Tanganyika Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipotembelea Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, New York Marekani tarehe 16 Julai, 1963. Mwalimu anamvika Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Bw. U Thant, pini maalum ambayo ni nembo ya mwenge wa uhuru. Wanaoshuhudia kutoka kushoto ni Bw. Oscar Kambona, Waziri wa Mambo ya Nje na Ulinzi wa Tanganyika, na kulia ni Balozi Chifu Erasto A.M. Mang'enya, Mwakilishi wa Kudumu wa Tanganyika Umoja Mataifa.

# Chifu Erasto Andrew Mbwana Mang'enya

### Chifu Wa Wabondei, Mwanadiplomasia, Spika Wa Bunge

*"Nyota Iliyong'ara Kitaifa na Kimataifa"*

Na Patson Sobha

*"Tanga, waja leo, kuondoka ni majaaliwa"* ni usemi unaosadifu ukarimu na roho nzuri waliyonayo wenyeji kwa Mkoa wa Tanga ukiwa na maana kwamba mgeni akifika mkoa huo, atakirimiwa kiasi kwamba hatataka kuondoka.

Mkoa wa Tanga umebarikiwa kwa mambo mengi ikiwemo chakula na hasa matunda, hali ya hewa nzuri – baridi kwa upande wa milimani na joto kiasi kwa upande wa ufukwe wa Bahari ya Hindi.



Uoto mzuri wa misitu minene, mashamba ya machungwa, maembe, kokoa, kahawa, mkonge, mito, maporomoko ya maji na Milima ya Usambara vinadhihirisha uzuri wa asili wa mkoa huo.

Mkoa wa Tanga una sifa nyingi mno zikiwemo kuwa makao makuu ya kwanza ya Serikali ya Mjerumani, makao makuu ya kwanza ya Jeshi la Mjerumani na Jeshi la Polisi, na pia sehemu ya kwanza kujengwa reli na bandari ya kwanza kusafirisha mazao ya kilimo hasa mkonge na kahawa kwenda nchi za nje.

Pamoja na mkoa wa Tanga kuwa na watu wakarimu, mkoa huo umebarikiwa pia kuwa chimbuko la watu mashuhuri na viongozi wengi wanaojulikana kitaifa na kimataifa. Miongoni mwa watu hao huwezi kumsahau Shabaan Robert, nguli wa mashairi, mtunzi na mwandishi mahiri wa vitabu.

Kwa upande wa siasa, utasikia jina la Kleist Sykes, mwanzilishi wa Chama cha TAA (Tanganyika African Association), mwanasiasa na mwanaharakati za uhuru wa Tanganyika, mfanyabiashara na mwanajeshi aliyepigana Vita vya Kwanza vya Dunia.

Ukizungumzia TAA ni lazima umkumbuke Hamza Kibwana Bakari Mwapachu, aliyekuwa Rais wa chama hicho cha harakati za wafanyakazi tawi la Tabora na baadaye akawa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje. Isivyo bahati mauti yalimkuta mapema sana mwaka 1962 ikiwa ni miezi tisa tu baada ya Uhuru wa Tanganyika akiwa na umri wa miaka 49 tu.

Wahenga walisema mtoto wa nyoka ni nyoka, pengine ndiyo maana watoto wa Hamza Kibwana Bakari Mwapachu aliyekuwa msomi wa Chuo Kikuu cha Makerere, ambao ni Harith Bakari Mwapachu aliyekuwa Waziri wa Wizara mbalimbali, na mdogo wake Balozi Juma Volta Mwapachu, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, walifuata nyayo za baba yao.

Watu wengine mashuhuri kutoka mkoa huo ni pamoja na Jaji Mkuu Mohamed Chande Othman, aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania kuanzia tarehe 28 Desemba 2010 – 18 Januari, 2017. Wengine ni Rashid Othman aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa kuanzia mwaka 2006 hadi 2013.

Ni Tanga pia ndiko alikozaliwa mwandiplomasia na Mhandisi Balozi John William Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi kuanzia tarehe 9 Machi, 2016 hadi 17 Februari, 2021 alipofariki dunia. Balozi Kijazi alikuwa pia Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wako viongozi wengi akiwemo Balozi Adadi Rajab, aliyekuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai, na Mbunge wa Muheza, jimbo ambalo kwa sasa linaongozwa na Mhe. Hamis Mwinjuma (Mwana FA), Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, huyu pia ni mwanamuziki mahiri.

Kwa makala hii, siwezi kumaliza kutaja watu wote mashuhuri kutoka Mkoa wa Tanga maana ni wengi mno waliosifika katika nafasi mbalimbali zikiwemo siasa, imani, elimu, muziki, utamaduni na michezo.

Makala hii itajikita zaidi kumzungumzia Mwanadiplomasia, Chifu wa Kabila la Wabondei, na Spika wa Bunge ambaye licha ya sifa zake kemkem, ni nadra sana kusikia akitajwa katika historia ya Tanzania, labda utembelee kumbi za Kamati za Bunge zilizoitwa kwa jina lake katika majengo ya Bunge ya Dodoma na Dar es Salaam, ama huenda Wilaya ya Muheza katika Shule ya Sekondari ya Erasto Mang'enya.

Katika miteremko ya Milima ya Usambara, Kijiji cha Mkuzi, Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga, wakati huo Tanganyika ikiwa chini ya ukoloni wa Wajerumani, tunakutana na familia ambayo kwao nyota njema ilionekana asubuhi. Nyota hii ilianza kung'aa baada ya familia ya mtumishi wa Mungu



**Balozi Chifu Erasto A.M. Mang'enya**, Mwakilishi mpya wa Kudumu wa Tanganyika na Zanzibar Umoja wa Mataifa akiwasilisha hati za utambulisho kwa Bw. U Thant, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ofisini kwake tarehe 17 Aprili, 1963.

**Mnamo mwaka 1967 Mang'enya alisafiri kwenda nchi za kijamaa**

**Ni wakati huo Rais Julius Nyerere alikuwa katika harakati za kueneza sera ya ujamaa, alimtuma Chifu Mang'enya kwenda katika nchi hizo zikiwemo Scandinavia, Ujerumani Mashariki na Umoja wa kisovyeti (Urusi) kujifunza namna ya utekelezaji wa sera hiyo.**

Canon Henry na Bibi Mary Eleanor Mang'enya kupata mtoto wa kwanza wa kiume aliyeitwa Erasto Andrew Mbwana Mang'enya.

### Kuzaliwa Kwake

Chifu Balozi Erasto Andrew Mbwana Mang'enya alizaliwa tarehe 17 Aprili, 1915 akiwa mtoto wa kwanza wa familia ya Mzee Henry Eleanor Mang'enya aliyekuwa kiongozi wa Kanisa la Anglikana.

### Safari ya Elimu

Erasto Mang'enya, alisoma masomo yake ya awali katika shule mbalimbali za Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar na Tanga kutoka mwaka 1919 hadi 1933. Shule hizo ni pamoja na Mkuzi, Magila, Kiwanda, na baadaye Shule ya Mafunzo ya Ualimu ya Minaki.

Mwaka 1934 alijiunga na chuo kilichojulikana kama King's College Budo, kilichokuwa chini ya Kanisa la Anglikana, Kampala, Uganda ambapo alifanya mtihani wa kujiunga na Chuo cha Makerere. Alisoma chuo hicho kuanzia mwaka 1935 hadi mwaka 1937 alipomaliza masomo yake.

### Kazi

Mnamo mwaka 1938 Erasto Mang'enya aliajiriwa katika Idara ya Elimu ya Tanganyika, ambayo kwa sasa ni kama Wizara ya Elimu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo alifundisha katika shule mbalimbali za sekondari.

Mwaka 1938 – 1943 alifundisha katika Shule ya Sekondari Malangali mkoani Iringa. Shule hii ni miongoni mwa shule kongwe ambazo zilitoa viongozi wa juu wa Serikali, na kati ya mwaka 1943 – 1947 alifundisha Sekondari ya Old Moshi mkoani Kilimanjaro.

Kati ya mwaka 1947 na 1952 Mang'enya alifundisha Shule ya Sekondari Tanga, na mwaka 1953 – 1957 Sekondari ya Tabora, na baadaye akahamia Shule ya Sekondari Songea mwaka 1958.

### Chifu wa Wabondei

Erasto A. M. Mang'enya alikuwa miongoni mwa Watanganyika wachache wasomi wenye shahada kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda, baadaye akawa mwanasiasa, mwanadiplomasia wa kitaifa na kimataifa, Naibu Spika, na Spika wa Bunge.

Alitawazwa kuwa Mtema (Chifu) wa Wabondei mwaka 1958, akiongoza Wabondei wanaopatikana katika miteremko ya Milima ya Usambara, Kaskazini – Mashariki mwa Tanganyika, eneo ambalo sasa linajulikana kama Wilaya ya Muheza na sehemu pia za Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga.

### Siasa

Mnamo mwaka 1960 aliingia rasmi katika Bunge la Tanganyika kwa tiketi ya chama kilichopigania Uhuru wa Tanganyika yaani Tanganyika African National Union (TANU) chini ya kiongozi wake Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na akachaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hilo, wakati huo Spika wa Bunge alikuwa A.Y.A Karimjee.

Mnamo mwaka 1962 wakati Tanganyika ilipokuwa Jamhuri kamili, aliteuliwa na Rais wa Tanganyika Mwalimu Julius Nyerere kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Mawasiliano, Nishati na Ujenzi.

### Balozi

Mapema mnamo 1963 alihamishiwa katika Wizara ya Mambo ya Nje na kupelekwa New York kama Mjumbe Maalum wa Tanganyika katika Umoja wa Mataifa na kuanzia Aprili 17, 1963 hadi 1964 alikuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanganyika katika Umoja wa Mataifa.

Chifu Mang'enya aliporejea Tanganyika kutoka Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1964, aliteuliwa kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii na Utamaduni wa Kitaifa. Aliongoza Wizara hiyo kwa mwaka mmoja hadi 1965.

Mwaka 1965 aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi ya Tanzania (Ombudsman), "Permanent Commission of Enquiry (PCE)" ambayo aliiongoza kwa miaka mitano hadi mwaka 1970.

Mnamo mwaka 1967 Mang'enya alisafiri kwenda nchi za kijamaa, ni wakati huo Rais Julius Nyerere alikuwa katika harakati za kueneza sera ya ujamaa, alimtuma Chifu Mang'enya kwenda katika nchi hizo zikiwemo Scandinavia, Ujerumani Mashariki na Umoja wa Kisovieti (Urusi) kujifunza namna ya utekelezaji wa sera hiyo.

Mwaka 1970 Chifu Mang'enya aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Mahakama Maalum ambayo ilisikiliza rufaa kwa malalamiko ya utaifishaji wa majengo mbalimbali hatua ambayo Serikali iliichukua kati ya mwaka 1967 na 1970 katika utekelezaji wa Azimio la Arusha la mwaka 1967.

Mnamo mwaka wa 1972 aliteuliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi "Permanent Commission of Enquiry (PCE)". Akiwa katika nafasi hiyo alitembelea nchi mbalimbali ikiwemo Australia, New Zealand na Israel.

## Spika wa Bunge

Chifu Erasto Andrew Mbwana Mang'enya alichaguliwa kuwa Spika wa Bunge na kuweka historia ya kuwa Spika wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihudumu katika nafasi hii tangu tarehe 20 Novemba, 1973 hadi 5 Novemba, 1975 alipomaliza muda wake na nafasi hiyo kurejea tena kwa Chifu Adam Sapi Mkwawa.

Chifu Mang'enya alishinda tena Ubunge kupitia Jimbo la Muheza katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 26, 1975, uchaguzi unaotajwa kuwa mgumu zaidi katika historia ya siasa za chama kimoja cha TANU kwani katika uchaguzi huu zaidi ya asilimia 75 ya waliokuwa Wabunge wa Bunge la Pili (1970 – 1975), walipoteza nafasi zao.

> **Baada ya kustaafu Ubunge mwaka 1980**
>
> **Chifu Erasto Mbwana Mang'enya hakuendelea na kazi ya kisiasa mpaka alipoaga dunia mnamo tarehe 4 Aprili, 1991**

Mang'enya alipomaliza Ubunge wake katika Bunge la Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1980, kiti cha Jimbo la Muheza kikachukuliwa na Luka Dunstan Kitandula.

Baada ya kustaafu Ubunge mwaka 1980, Chifu Erasto Mbwana Mang'enya hakuendelea na kazi ya kisiasa mpaka alipoaga dunia mnamo tarehe 4 Aprili, 1991.

## Mambo ya Kukumbukwa

Watanzania na dunia tunayo mengi ya kukumbuka na kujifunza kutoka kwa Chifu Erasto Andrew Mbwana Mang'enya kutokana na maisha yake akiwa kiongozi wa kabila la Wabondei, mtumishi wa umma, mwanasiasa, na mwanadiplomasia.

Mchango wa Chifu Mang'enya katika Elimu ulikuwa nguzo ya maendeleo kwani alifundisha katika shule mbalimbali za sekondari kwa zaidi ya miaka 20, akiwalea viongozi wa baadaye wa taifa. Akiwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Old Moshi, na shule zingine, alihamasisha nidhamu, uzalendo, na ubora wa kitaaluma. Aliamini kuwa elimu ni silaha ya ukombozi wa fikra na maendeleo ya kijamii.

Katika uongozi wa jadi, akiwa Chifu Mkuu wa Wabondei, Chifu Erasto Mang'enya aliheshimu na kuendeleza mila za jamii yake na alijenga daraja kati ya utawala wa jadi na Serikali ya kisasa, akihamasisha maendeleo bila kupoteza utambulisho wa kitamaduni, na alidhihirisha kuwa uongozi wa jadi ni mshirika wa maendeleo ya kisasa.

Kidiplomasia, tutamkumbuka Chifu Mang'enya kama mtu aliyewakilisha Taifa la Tanzania likiwa bado changa na kusaidia kuwakilisha maslahi ya taifa akihimiza ushirikiano na amani, kwa kufanya hivyo aliwezesha kuunda taswira ya taifa jipya lenye dira ya kimataifa.

Maisha ya Chifu Erasto Andrew Mbwana Mang'enya yalikuwa tunu kwa Taifa la Tanzania, kizazi cha sasa na baadaye hatuna budi kumkumbuka na kudumisha yale yote aliyoyatenda kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu.

Ni muhimu kuwakumbuka Watanzania waliotumikia taifa kwa umahiri, uaminifu na na uzalendo wa hali ya juu. Tuwakumbuke maana kadri unavyojua kuhusu yaliyopita, ndivyo kadri unavyoweza kujiandaa vema kwa ajili ya yajayo. Hayo ni maneno aliyoyasema Rais wa 26 wa Taifa la Marekani Bw. Theodore Roosevelt (1858 – 1919)



# Job Yustino Ndugai: Ameacha Alama Isiyofutika Katika Historia Ya Bunge La Tanzania

*Na. Zuhura Mtatifikolo*

**MAISHA ya mwanadamu ni hadithi. Hadithi yenye mwanzo, sura, na mwisho wake, na yenye nyakati za furaha, changamoto na mafanikio.**

**Hadithi ambayo kila binadamu huandika kwa matendo, uadilifu na huduma kwa wengine. Wapo wanaoandika hadithi za muda mfupi, na wapo wachache wanaoacha simulizi zinazodumu vizazi na vizazi.**

**Miongoni mwa hao ni Job Yustino Ndugai, Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye safari yake ya maisha imebaki kuwa hadithi ya uongozi, uthubutu na uadilifu.**

## Siku Iliyobadilisha Historia

Jumatano ya Agosti 6, 2025, itabaki kwenye kumbukumbu za Taifa kama siku ambayo jina la Job Ndugai lilipokea ubatizo wa milele.

Ilikuwa siku iliyohitimisha safari yake ya miaka 62 na miezi saba duniani, sawa na takribani siku 22,886 za maisha ya utumishi na kujitolea.

Taarifa ya Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma katika Ofisi ya Bunge, ilisema "Kwa masikitiko makubwa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, anatangaza kifo cha Spika Mstaafu Job Yustino Ndugai kilichotokea leo tarehe 6/8/2025 Jijini Dodoma. Taratibu za mazishi zinaendelea kwa kushirikiana na familia, na taarifa kamili itatolewa."

Hadi umauti unamkuta Ndugai alikuwa ameshinda kura za maoni katika mchakato wa Ubunge Chama Cha Mapinduzi wa kumpata mgombea wa Ubunge wa Jimbo la Kongwa.




Allibuka mshindi kwa kupata kura 5,690 akiwashinda Ngaya Mazanda 195, Emmanuel Mbena 232, Pascal Mahinyila 321, Philipo Chiwanga 358, Elias John 435, Simon Ngatunga 517, Samora Mshana 544, Deus Seif 1,260 na Isaya Mngurumi 2,602.

## Uongozi Ndani ya Bunge

Safari yake ya kibunge ilikuwa ndefu na ya mafanikio. Alianza kama Mwenyekiti wa Bunge katika Bunge la Tisa (2005 – 2010) chini ya Spika Marehemu Samuel Sitta, nafasi iliyomjenga katika misingi ya uongozi wa Bunge.

Mwaka 2010, alichaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Kumi (2010 – 2015) chini ya Mhe. Anne Makinda, mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Spika wa Bunge. Mwaka 2015, Hayati Ndugai alichaguliwa kuwa Spika wa Bunge la 11 (2015 – 2020) kwa kura 254.

Mwaka 2020, alirudi tena kuongoza Bunge la 12 (2020 – 2025), lakini Januari 6, 2022, alitangaza kujizulu nafasi hiyo kwa hiari yake, akiacha mfano wa kiongozi anayeheshimu taasisi na maamuzi yake binafsi. Nafasi yake ilichukuliwa na Dkt. Tulia Ackson, aliyekuwa Naibu Spika wake kwa miaka saba.

Kwa miaka yake yote Bungeni, Ndugai alitumikia Mabunge manne mfululizo yaani Bunge la 9, 10, 11 na 12 jambo linalomweka kwenye rekodi ya viongozi waliotumikia muda mrefu zaidi katika historia ya Bunge la Tanzania.

## Mageuzi Ndani Ya Bunge

Miongoni mwa mambo yatakayodumu kama kumbukizi ya Ndugai ni jinsi alivyoongoza mageuzi makubwa katika uendeshaji wa shughuli za Bunge.
Ikumbukwe katika Bunge 11 Ndugai aliongoza Kamati ya Bunge iliyozunguka duniani kwenye mabunge mbalimbali kujifunza jinsi ya uendeshaji wa shughuli zao na ndipo akaongoza jopo la utungaji wa kanuni.

Ndugai ndiye aliyesimamia kuandaliwa kwa Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo kwa sasa ni Kanuni za 2023, zilizoleta mfumo bora na wa kisasa wa usimamizi wa shughuli za Bunge.

Katika uongozi wake, alisisitiza umuhimu wa Wabunge kujifunza kutoka mabunge ya nchi nyingine. Mara kadhaa aliwatuma Wabunge kujifunza mifumo ya uendeshaji wa mabunge ya kisasa duniani, jambo lililosaidia kuimarisha uwajibikaji na ufanisi.




Ndugai pia alijulikana kwa msimamo wake usioyumba kuhusu uhuru wa Bunge na alisisitiza kuwa Bunge ni mhimili huru unaopaswa kuheshimiwa.

Katika uhai wake, Ndugai aliwahi kuanzisha kamati nne za Bunge zilizoangazia udhibiti wa rasilimali kama almasi, tanzanite, gesi asilia na uvuvi wa bahari kuu. Mapendekezo ya kamati hizo yalisaidia kuongeza mapato ya Serikali.

Kadhalika, Ndugai atakumbukwa kwa kufanikisha ujenzi wa Shule ya Wasichana ya Bunge iliyoko Kikombo, Dodoma, mradi uliotekelezwa kwa michango ya Wabunge na wadau, kama ishara ya uwekezaji katika elimu ya mtoto wa kike.

### Alichosema Rais Samia

Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiongoza hafla ya Kitaifa ya Mazishi ya Hayati Ndugai, alisema kifo cha Ndugai ni pigo kwa taifa, akimtaja marehemu kama kiongozi shupavu, mzalendo na mkomavu kisiasa ambaye mchango wake utaendelea kuishi katika mioyo ya Watanzania.

"Tumepoteza nguzo muhimu, aliyeaminiwa ndani na nje ya nchi, aliyejituma bila kuchoka katika kulinda maslahi ya Taifa letu," alisema.

Alisema, Hayati Ndugai aliongoza mageuzi makubwa, ikiwemo kuingiza Bunge katika mfumo wa kidijitali kupitia Bunge Mtandao, mfumo uliowezesha shughuli za Bunge kufanyika kisasa zaidi, kwa ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji.

Aidha, Rais Dkt. Samia anamkumbuka Ndugai kwa kusimamia ukamilishaji kwa Jengo la Utawala Annex lenye kumbi tisa za kisasa za mikutano, pamoja na kuanzisha Kamati Maalum Nne za ushauri kwa Serikali kuhusu rasilimali muhimu za taifa kama almasi, tanzanite, gesi na uvuvi wa bahari kuu.

"Mapendekezo ya kamati hizi yalisaidia kuimarisha usimamizi wa rasilimali na kuongeza mchango wake kwenye pato la taifa," aliongeza Rais Dkt. Samia.

Rais Dkt. Samia pia alikumbusha nafasi ya Ndugai katika mchakato wa kutungwa kwa sheria ya kuitambua Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi. Mwaka 1973 Mwalimu Julius Nyerere alitangaza kuwa Dodoma ndiyo makuu ya nchi lakini hakukuwa na sheria iliyotungwa.

### Anavyokumbukwa na Viongozi

Spika Mstaafu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson alimtaja Hayati Ndugai kama mwalimu na kiongozi thabiti.

"Nilijifunza mengi kwake, hasa msimamo wake katika mambo yenye maslahi kwa Taifa. Hakuwa mtu wa kuyumbishwa, hakupenda kuona mtu akionewa. Nitamkumbuka kwa uthubutu na upendo wake kwa watu," alisema.

Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, na Jaji Mkuu, Mheshimiwa George Masaju, walimuelezea marehemu kama mpenda haki, aliyeamini katika utawala bora, na



aliyesimamia vizuri matumizi ya rasilimali za taifa kupitia kamati maalum za ushauri Bungeni. Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa George Simbachawene, alisema Ndugai alikuwa kiranja wa siasa wa Wabunge wa Dodoma.

Alisema amepoteza rafiki yake na ana mchango mkubwa katika siasa zake na ni kiongozi wa mfano.

“Katika historia yangu ya siasa anao mchango mkubwa tulianza kugombea pamoja mwaka 2000, mimi nikakosa na ukumbuke tunatoka Mkoa mmoja.

“Nilipopata mwaka 2005 nilimkuta yeye ni mzoefu kwa hiyo aliniongoza namna ya kwenda wakati wa michujo na nitakumbuka siku majina yetu yanajadiliwa kwenye Kikao cha Kamati ya Siasa ya Mkoa, Kamati ilikuwa ina hati hati ya kuniteua ingawa niliongoza kwa kura.”

“Hapo ndipo naukumbuka mchango wa Ndugai kama rafiki na katika sehemu yangu ya maisha ya kisiasa, kwa sababu alisema kaza moyo usije ukanyang’awa ushindi pambana,”alisema.

Katika siasa za kitaifa, anasema Ndugai atakumbukwa kwa alivyofanya mageuzi makubwa kwenye Kanuni za Bunge ambazo zinatumika hadi sasa na kwamba zimefanya Bunge kuwa lenye meno.

“Kilicholala sio mwili tu bali ni jabali la maendeleo kwa Mkoa wa Dodoma, katika Bunge 11 liliongozwa na Marehemu Samuel Sitta, Ndugai alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge alizunguka duniani kwenye mabunge mbalimbali kujifunza jinsi ya uendeshaji wa shughuli zao na ndipo akaongoza jopo la utungaji wa kanuni,”anasema.

Anasema atakosa mawazo na mchango wa mwanasiasa huyo ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma na mtu makini mwenye misimamo yake.

“Enzi za uhai wake Ndugai aliamini na kusimamia haki na hakuwa tayari kuona haki inapotezwa na mtu,”anasema.

Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Kondoa Mjini, Mhe. Mariam Ditopile, alisema Ndugai alikuwa ni kiongozi aliyeipenda nchi yake kwa dhati na aliipenda sana Dodoma.

Mbunge wa Mtumba, Mhe. Anthony Mavunde, anaeleza Ndugai alitamani kuona maendeleo ya Dodoma yanakua kwa kasi kubwa na watoto wa Dodoma wanapata elimu bora.

“

**Ndugai alikuwa mwalimu wa siasa kwa wengi na atakumbukwa kwa misimamo yake ya kuamua mambo hasa kunapotokea mkwamo.**

*Mbunge wa Mvumi Mhe.* ***Livingstone Lusinde*** ”

Mbunge wa Mvumi Mhe. Livingstone Lusinde alisema Ndugai alikuwa mwalimu wa siasa kwa wengi na atakumbukwa kwa misimamo yake ya kuamua mambo hasa kunapotokea mkwamo.

### Safari ya Elimu na Uongozi

Hayati Job Yustino Ndugai alizaliwa katika kitongoji cha Mtale, Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma. Elimu yake ya msingi aliipata kijijini kwao, kisha akaendelea na elimu ya sekondari katka Shule ya Sekondari Kibaha na baadaye shule ya Sekondari Old Moshi, shule ambazo kwa miaka mingi zimekuwa zikichukua wanafunzi wenye ufaulu wa juu kitaifa.

Baada ya hapo alisoma katika vyuo mbalimbali ikiwemo Chuo cha Wanyamapori Mweka, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na vyuo vya nje ya nchi vya Norway, akionesha kiu ya kupata maarifa mapana kuhusu uongozi, uhifadhi na masuala ya kijamii.

Akiwa mtumishi Serikalini katika Wizara ya Maliasili na Utalii, Ndugai alijulikana kwa uadilifu na uwajibikaji. Mwaka 2000 aliamua kuacha utumishi na kuingia kwenye siasa.

Aligombea Ubunge wa Jimbo la Kongwa kupitia CCM, nafasi aliyoshinda na kuendelea kuishikilia kwa miaka 25 mfululizo hadi mauti yalipomfika.

**Historia ya Bunge la Tanzania haiwezi kukamilika bila kutaja jina la Job Yustino Ndugai. Alikuwa Spika mwenye dira, Mbunge wa mfano na Mtanzania aliyelitumikia Taifa lake kwa moyo wa kujitolea na uwajibikaji.**

### Safari ya Mwisho


Licha ya kuwa msiba wake ulitokea kipindi ambacho Bunge lilikuwa limevunjwa kwa mujibu wa Katiba, mamia ya viongozi na Wabunge wa zamani walifurika Dodoma na Kongwa kushiriki maziko.

Mazishi yalifanyika Jumanne, Agosti 12, 2025, kijijini kwake Mandumbwa, yakiongozwa na aliyekuwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa, aliyewasilisha salamu za rambirambi kwa niaba ya Serikali.

Alikuwa mtu wa imani, aliyeamini katika kufanya kazi kwa bidii na kuacha matokeo yawe mashahidi wake.

Kwa hakika, historia ya Bunge la Tanzania haiwezi kukamilika bila kutaja jina la Job Yustino Ndugai. Alikuwa Spika mwenye dira, Mbunge wa mfano na Mtanzania aliyelitumikia Taifa lake kwa moyo wa kujitolea na uwajibikaji.

Urithi wake utaendelea kuishi katika taasisi alizozisimamia, sheria na kanuni alizoanzisha, na mioyo ya wale wote aliowagusa.



# Mkataba Wasainiwa Ujenzi wa Hoteli ya CPA Dodoma




*Na. Deonisius Simba*

**Hatimaye ndoto ya Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika imetimia na sasa wameanza ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano Jijini Dodoma.**

**Mafanikio hayo yamekuja baada ya CPA Kanda ya Afrika kusaini Mkataba wa Ujenzi ya Hoteli ya Nyota Tano na Kampuni ya CRJE (East Africa) Limited kutoka nchini China na tayari kazi imeanza.**

Mkataba huo wa ujenzi umesainiwa na Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Uwekezaji ya CPA Kanda ya Afrika (Commonwealth Investment Company Limited - CICL), Mhe. Dkt. Tulia Ackson na Mwakilishi wa Mkandarasi kutoka Kampuni ya CRJE (East Africa) Limited, Ndugu Lu Chunbao na kushuhudiwa na baadhi ya viongozi

Katika mazungumzo yake Dkt. Tulia alimtaka mkandarasi kuhakikisha ujenzi huo unafanyika kwa wakati na ubora unaotakiwa kwani ni muhimu kwa Umoja huo na Taifa.

Mkataba huo unataja kuwa utakwisha ndani ya miezi 22 kama ambavyo wamekubaliana kabla na baada ya kutiliana saini ingawa wahusika wangetamani uishe hata kabla ya muda.

Aidha Dkt. Tulia aliishukuru Serikali kupitia Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa kutoa ardhi na vibali vyote vilivyoruhusu ujenzi wa hoteli hiyo kuanza ambayo itajengwa eneo la Njedengwa katika Jiji la Dodoma.

"Ujenzi wa hoteli hii ambayo ni ya kwanza ya Nyota Tano Jijini Dodoma unaendana na mpango wa Serikali wa kukamilisha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato ambapo vinategemeana," alisema Dkt. Tulia.

Kwa mujibu wa Dkt. Tulia, wageni wengi watashuka na kufikia katika hoteli hiyo ikiwemo wageni wanaokuja kuonana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa shughuli za kiserikali.

Kiongozi huyo alisema CPA Kanda ya Afrika inatambua mchango wa Spika Mstaafu na Mwenyekiti wa



**Mweka Hazina wa CPA Kanda ya Afrika ambaye ni Mbunge kutoka Bunge la Uganda, Mhe. Enos Asiimwe alisema Hoteli hiyo ni mradi wa kwanza kutekelezwa na umoja huo na kwamba ni matumaini yao mradi huo utakuwa na mafanikio makubwa,".**

Bodi Mstaafu wa Kampuni wa CICL Hayati Job Ndugai katika ujenzi wa hoteli kwa jinsi alivyopigania mradi huo.

Alisema wakati huo Hayati Ndugai akiwa Mwenyekiti wa Bodi ya CICL ndiye alishawishi ujenzi wa kitega uchumi hicho kufanyika nchini Tanzania ambako ndipo yalipo Makao Makuu ya CPA Kanda ya Afrika.

Kwenye mkataba huo, Benki ya CRDB imeingia ubia kwa kukubali kushiriki katika ujenzi wa hoteli hiyo ambayo itakuwa moja ya kivutio kwa Jiji la Dodoma.

Naye Mweka Hazina wa CPA Kanda ya Afrika ambaye ni Mbunge kutoka Bunge la Uganda, Mhe. Enos Asiimwe alisema hoteli hiyo ni mradi wa kwanza kutekelezwa na umoja huo na kwamba ni matumaini yao mradi huo utakuwa na mafanikio makubwa.

Mhe. Asiimwe aliitaka Kampuni ya CRJE kufanya kazi kwa mujibu wa mkataba na akaomba isiwaangushe katika kutekeleza mradi huo ili umalizike kwa wakati.

Awali Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Katibu wa Kampuni ya CICL, Ndugu Baraka Leonard aliwashukuru washiriki wote wa hafla hiyo ya kutiliana saini na kueleza kuwa mradi huo wa hoteli utaacha alama kubwa ndani ya CPA na kuimarisha umoja huo kwa kuongeza mapato ya CPA.

Ndugu Leonard aliahidi kuwa karibu kwa uangalizi wa hatua zote kuanzia mwanzo hadi ukamilishaji wa mradi huo ambao unasubiriwa kwa hamu.



# Utaratibu Rasmi wa Wabunge Walio Wachache Bungeni katika Mabunge ya nchi za Kidemokrasia

*Na. Athuman Hussein, ndc*
a.brambati@bunge.go.tz

**Utaratibu rasmi wa Wabunge Waliowachache Bungeni unatokana na misingi ya demokrasia ya kiliberali. Aina hii ya demokrasia inachanganya uamuzi wa wengi (majority rule) na uhakika wa haki na uhuru wa waliowachache (minority). Katika demorasia ya aina hii, mambo ya msingi yanayopewa nguvu ni pamoja na uhuru wa kutoa maoni ya kisiasa, wingi wa mitazamo ya kisiasa inayotofautiana na ushiriki wa makundi anuai ya wananchi.**

Utaratibu huu unasisitiza mchakato wa demokrasia kuliko matokeo ya demokrasia kama alivyofafanua Profesa wa Marekani, Robert Dahil. Katika misingi mitano ya demokrasia iliyotolewa na mtaalamu huyu wa sayansi ya siasa, upo msingi mmoja unaohusu ushiriki unaofaa (effective participation). Kwa ufafanuzi wake, ushiriki unaofaa ni msingi wa kidemokrasia unaohitaji kila raia apate fursa stahiki ya kushiriki mijadala ya kisiasa na uamuzi unaofikiwa.

Kwa msingi huo, hakuna kundi la watu linaloweza kuwazuia wengine kushiriki mjadala au kufinya fursa ya wengine au kundi lingine kutoa maoni yao. Kwa maelezo hayo demokrasia ya Bungeni inahitaji kuwezesha majadiliano endelevu kwa namna inayotoa fursa kwa makundi yote ya kisiasa Bungeni kupata fursa ya kutoa maoni, mawazo na kushiriki ifaavyo katika mchakato wa kibunge. Kwa maneno mengine Wabunge waliowachache wanahitaji uhakika wa fursa ya kutoa maoni yao na kusikilizwa licha ya uchache wao.

Hayo yote kwa pamoja yanajenga msingi wa utaratibu wa kutoa nafasi rasmi kwa Wabunge wanaotokana na Chama chochote chenye Wabunge waliowachache ambapo katika mabunge mengine wanaitwa Wabunge wanaotoka Kambi ya Upinzani. Utaratibu huu kwa wakati wa sasa duniani umekuwa maarufu na unasisitizwa zaidi na waliberali pamoja na wanademokrasia wengine.

Kiasili, ipo misingi mikuu miwili ya utaratibu rasmi wa ushiriki wa Wabunge waliowachache Bungeni, katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge. Misingi hiyo inatokana na msisitizo wa kidemokrasia ya wingi wa maoni. Aina hiyo ya demokrasia inatambua kwamba, mamlaka na ushawishi wa kisiasa (political power and influence) yanagawanyika kati ya makundi mengi yanayotofautiana maoni na mitazamo, badalaa ya kuwa chini ya nguvu ya Kundi la wengi wenye mtazamo mmoja.

Msingi wa kwanza ni utofauti wa kisiasa (pluralism). Msingi huu, unataka Bunge litambue kwamba, ni halali kuwa na mitazamo mbalimbali inayotofautiana kutokana na kuwepo kwa tofauti za kisiasa nje ya Bunge husuan ndani ya nchi. Tafsiri yake ni kwamba, katika utekelezaji wa majukumu yake, Bunge linapaswa kutambua kuwa Wabunge wanaotokana na vyama vya siasa vyenye uwakilishi mdogo wanaweza kuwa na maoni tofauti na wale wa chama chenye Wabunge wengi.

"

Katika muktadha wa kibunge, Serikali huundwa na chama chenye Wabunge wengi.

Hivyo, jukumu la kufuatilia na kuhoji kwa ukamilifu utekelezaji wa shughuli za Serikali huangukia zaidi kwa Wabunge wanaotokana na vyama vyenye uwakilishi mdogo. Kwa nafasi hii, wao ndio wanaotekeleza wajibu wa msingi wa kuisimamia Serikali, kuhakikisha uwazi, uadilifu na uwajibikaji katika utendaji wa Serikali ndani ya mfumo wa kibunge. "

Kwa kuzingatia kanuni ya utofauti wa siasa (*pluralism)*, Bunge linawajibika kuwa na mfumo wa kiutendaji unaotambua, kulinda na kuruhusu nafasi ya Wabunge wa vyama vyenye uwakilishi mdogo. Lengo lake ni kuwezesha mitazamo yao isikike na kupata fursa ya kuzingatiwa katika mchakato wa uamuzi wa kibunge kwa mujibu wa misingi ya utawala wa kidemokrasia.

**Msingi wa pili** ni dhana ya uwajibikaji (*accountability*). Kwa mujibu wa msingi huu, wanaoshika madaraka ya kuongoza shughuli za umma wanapaswa kufuatiliwa, kuhojiwa na kutoa maelezo ya kina kuhusu mantiki ya uamuzi wao wowote, hatua wanazochukua na matokeo ya utekelezaji wa majukumu yao. Kwa mtazamo wa waliberali, wanaofanya kazi hii ni wale ambao hawapo madarakani na ambao, kwa misingi ya demokrasia, wanahusika kuhakikisha kuwa matumizi ya madaraka hayaendi nje ya mipaka ya sheria, maslahi ya wananchi na maadili ya uongozi.

Katika muktadha wa kibunge, Serikali huundwa na chama chenye Wabunge wengi. Hivyo, jukumu la kufuatilia na kuhoji kwa ukamilifu utekelezaji wa shughuli za Serikali huangukia zaidi kwa Wabunge wanaotokana na vyama vyenye uwakilishi mdogo. Kwa nafasi hii, wao ndio wanaotekeleza wajibu wa msingi wa kuisimamia Serikali, kuhakikisha uwazi, uadilifu na uwajibikaji katika utendaji wa Serikali ndani ya mfumo wa kibunge.

Dhanio (Assumption) katika mtazamo huu, ni kwamba, wajibu walionao Wabunge ni kwa vyama vyao vya siasa tu. Mtazamo huu hauzingatii wajibu wa Mbunge kwa wapiga kura wake, wala wajibu wake kwa taifa kwa ujumla, na haujali dhamira binafsi ya Mbunge katika utekelezaji wa majukumu yake. Licha ya upungufu huu, msingi huu bado ni muhimu katika Bunge kwani unaweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa Wabunge wa vyama vyenye uwakilishi mdogo wanazingatiwa na kushirikishwa katika michakato ya kibunge bila kujali dhana zilizopo.

Kutokana na maelezo hayo, suala la kuwa na utaratibu wa Bunge kutambua Wabunge waliowachache Bungeni limepewa msisitizo katika demokrasia ya kibunge. Wapo wanaowatambua Wabunge hao kwa jina "Wabunge waliowachache Bungeni (*Minority*). Mfano ni Mabunge ya Ghana, Marekani na Nigeria.

Mabunge ya nchi nyingine yanatumia Wabunge wa Kambi ya Upinzani (*Opposition*). Mfano ni nchi kama Australia, Uganda na Zimbabwe. Katika maana ya nje ya jina "Upinzani" na "Walio wachache" inaonekana kuna tofauti. Wanaotumia jina "Upinzani Bungeni" wameweka msisitizo kwenye upingaji wa maoni kwa maana ya upinzani. Lakini wanaotumia jina "Waliowachache Bungeni " wanasisitiza idadi ya wenye maoni hayo kuliko kupinga au kuunga mkono.

Pamoja na tofauti hizo za kisemantiki, majina hayo ama Kambi ya "Walio wachache Bungeni", au Kambi ya "Upinzani Bungeni" yana misingi inayofana. Misingi hiyo inatokana na kiini chake katika uliberali na demokrasia ya Vyama vingi katika uendeshaji wa nchi. Tofauti hiyo inaweza kuelezeka kwa namna tatu.

**Kwanza**, majina yote yanaonesha Wabunge wanaotokana na Vyama visivyounda Serikali. Kwa kuwa Chama kinachounda Serikali kina Wabunge wengi, vyama visivyounda Serikali ni vyama vyenye Wabunge wachache. Aidha, kutokana na chama chenye Wabunge wengi kujulikana kama Chama Tawala, Vyama vyenye Wabunge wachache vinajulikana kama Vyama vya Upinzani. Utambulisho huo unasababisha Wabunge watokanao na Vyama vya upinzani kujulikana kwa jina la Kambi ya Upinzani Bungeni (*Opposition*).

**Pili,** Kwa misingi mikuu miwili ya utaratibu rasmi wa ushiriki wa Wabunge waliowachache Bungeni iliyoelezwa awali, iwe Kambi ya Upinzani au Kambi ya waliowachache, Mabunge yanahitaji kuweka utaratibu rasmi wa uendeshaji wake. Utaratibu huo

unatambua muungano wa vyama zaidi ya kimoja Bungeni au chama kimoja cha Upinzani chenye Wabunge wengi miongoni mwa vyama vya Upinzani. Yote hiyo ni kuhakikisha kuna utaratibu rasmi wa kupata maoni na mawazo mbadala kutoka kwa Wabunge walio wachache au Kambi ya Upinzani Bungeni.

**Tatu**, aina hizo za majina ya Wabunge wasio kwenye Chama kinachounda Serikali, inatambua utamaduni wa uwajibikaji wa Serikali kuwekwa chini ya uongozi wa Wabunge walio wachache au Upinzani. Asili yake ni kutambua msingi wa pili wa utaratibu rasmi wa ushiriki wa Wabunge waliowachache ambao ni dhana ya uwajibikaji. Katika hili, mabunge mengi yametenga nafasi ya uongozi wa Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za Umma chini ya Kambi ya walio wachache (*Minority*) au Kambi ya Upinzani (*Opposition*).

Mfano, Katika Bunge la Ghana Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali inapaswa kuongozwa na Mbunge kutoka upande wa Kambi ya Waliowachache na Bunge la Zimbabwe Kamati kama hiyo inaongozwa na Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani.

> **Mfano wa nchi zenye Mabunge ambayo Kamati za Bunge Zinazosimamia Matumizi ya Fedha za Umma zinaongozwa na Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani au Walio wachache ni Tanzania, Uganda, Bangladesh na nyingine nyingi. Lakini zipo pia baadhi ya nchi zenye utaratibu tofauti kama vile Rwanda, Ethiopia, Msumbiji, Ujerumani, Ufaransa na Japan, kutaja baadhi.**

Mantiki ya Kamati hizo kuongozwa na Kambi ya Upinzani au ya Waliowachache ni imani ya umma, uhuru wa kisiasa za kivyama Bungeni na uhakika wa maoni mbadala. Mambo yanashadidia uongozi wa kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma kuwa chini ya Kambi ya Wabunge Waliowachache au Kambi ya Upinzani Bungeni. Kambi hiyo inaonekana kuwa na fursa stahifu ya kufanya uangalizi wa kina wa matumizi ya fedha za umma.

Mtazamo wa kiliberali kuhusu demokrasia Bungeni unachukulia kuwa, usimamizi madhubuti wa kibunge unahitaji uhuru wa Wabunge dhidi ya maelekezo na shinikizo la chama cha siasa. Ukuu wa Katiba nao unatazama misingi ya Katiba katika usimamizi wa kibunge. Vyote kwa pamoja havipangani katika umuhimu wa kuwa na usimamizi thabiti wa kibunge wa shughuli za Umma. Hivyo, Kambi ya waliowachache au Kambi ya Upinzani kuongoza Kamati zenye jicho kali kwenye matumizi ya fedha za umma ni jambo linaloungwa mkono na mitazamo yote miwili ambayo ni ukatiba na uliberali.

Mfano wa nchi zenye Mabunge ambayo Kamati za Bunge Zinazosimamia Matumizi ya Fedha za Umma zinaongozwa na Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani au Walio wachache ni Tanzania, Uganda, Bangladesh na nyingine nyingi. Lakini zipo pia baadhi ya nchi zenye utaratibu tofauti kama vile Rwanda, Ethiopia, Msumbiji, Ujerumani, Ufaransa na Japan, kutaja baadhi.

Kwa Tanzania, historia ya utaratibu huu inajambo la kuarifu uzoefu uliopo. Ni uzoefu muhimu katika kuelewa masuala ya Kibunge na desturi za Bunge la Tanzania. Uelewa huo, unaweza kuwa ngao dhidi ya mitazamo potofu au maelezo yasiyosahihi yanayotolewa na watu mbalimbali. Aidha, ufafanuzi huo unaweza kuwa nyenzo ya kujenga msingi madhubuti wa kila mtu kuwa na mawazo yenye mashiko.Kwa sababu hiyo, toleo lijalo litafafanua historia ya utaratibu wa Bunge kutambua Wabunge walio wachache au kambi ya Upinzani Bungeni.

Mwanafalsafa Confucius ambaye kwa kichina anajulikana kama Kǒng Fūzǐ aliwahi kusema "**Soma yaliyopita ikiwa unataka kueleza yajayo**." Kwa upande wa busara za Pwani ya Afrika Mashariki, upo msemo kwamba, "**Mizizi ya mti haioti siku ya kwanza, bali huvumilia mvua na jua hadi kutokea tunda.**" Yote hayo yanasisitiza wasomaji wa makala hii kujiandaa kusoma bila kukosa mwendelezo wa Makala hii katika Toleo lijalo.

# Uwajibikaji wa Mbunge



*Na. Athuman Hussein, ndc*
*a.brambati@bunge.go.tz*

Uwajibikaji ni kiini cha ufanisi wa kila Bunge duniani. Ufanisi huo unategemea uwajibikaji wa Mbunge mmoja mmoja na Wabunge kwa ujumla wao. Kutokana na hayo, linaibuka swali la msingi na muhimu. Swali hilo ni: "Uwajibikaji wa Mbunge ni nini? Pengine inaweza kuvutia kufahamu "Nini hasa maana ya Mbunge kuwajibika?"

Kwa uhakika, kadiri wananchi wanavyokuwa na uelewa mpana zaidi kuhusu masuala ya kibunge, ndivyo matarajio yao kuhusu uwazi katika masuala ya Bunge na uharaka wa kupata majibu unavyongezeka. Mara nyingi mitazamo ya umma kuhusu Bunge haitokani tu na sheria ambazo Bunge linazipitisha, bali pia uadilifu, bidii na uwajibikaji wa wale wanaowawakilisha.

Kwa Wabunge, uwajibikaji si tu ni wajibu wa kikatiba, bali pia ni msingi wa kuaminika, uhalali wa kisiasa na uwakilishi wenye tija. Uwajibikaji ni kiamuzi (determinant) cha ubora wa uchambuzi wa miswada ya sheria, nguvu ya Bunge kuisimamia Serikali na afya ya utawala wa kidemokrasia. Mbunge anapothamini uwajibikaji, analijengea heshima Bunge. Lakini anapoupuuza uwajibikaji, anachangia kudhoofisha imani ya wananchi kwa Bunge.

Makala hii inaangazia uwajibikaji wa Mbunge kwa kuchambua dhana yenyewe na utekelezaji wa majukumu ya Bunge. Maelezo yatagusa umuhimu wa uwajibikaji wa Mbunge, maana yake kadhalika na ngazi mbalimbali za uwajibikaji wa Mbunge.

Kwa kuanzia, dhana ya "Uwajibikaji wa Mbunge" inawakilishwa kwa neno moja la msingi ambalo ni "Uwajibikaji". Prof. Mlacha katika Kamusi ya Sheria, Kiingereza – Kiswahili, ukurasa wa 4, ameonesha kuwa "Uwajibikaji" ni neno la Kiswahili ambalo kwa kiingereza ni "accountability".

Kwa upande wao, Prof. James Salehe Mdee, Prof. Kimani Njogu na Bwana Adam Shafi katika Kamusi ya Karne ya 21, Kamusi ya Kiswahili yenye uketo zaidi katika karne hii, wameonesha kwamba,

uwajibikaji ni hali ya kusimamia na kufanya kazi kwa ukamilifu. Kwa kuzingatia hayo, uwajibikaji wa Mbunge ni uzingatiaji wa wajibu wa Mbunge wa kikatiba na kijamii unaomtaka kueleza, kufafanua na kutoa majibu. Wajibu huo ni kuhusu uamuzi, hatua na mwenendo wake kwa Bunge, kwa Chama chake cha siasa, kwa nchi yake na kwa dhamira yake mwenyewe.

Fasili hiyo inasukuma ufafanuzi wa dhana ya "uwajibikaji wa Mbunge" kwa kuangalia uhusiano alionao Mbunge. Uhusiano unaohusika hapa ni baina ya Mbunge na wahusika wengine unaoelezeka katika aina tano za uwajibikaji.

**Kwanza ni uwajibikaji kwa wapigakura**. Mbunge yeyote aliyechaguliwa anao wajibu wa kuwasikiliza, kuwawakilisha na kurudisha mrejesho kwa wapigakura wake. Lengo ni kuhakikisha kuwa mahitaji yao yanazingatiwa, kuwasilishwa panapostahili na kufuatiliwa.

Msingi wa uwajibikaji wa Mbunge kwa wapigakura wake, unatokana na sababu za Mbunge kupata ubunge. Wapigakura ndio waliomwezesha Mbunge kuwa katika nafasi hiyo. Kwa Mbunge kutowajibika kwa wapigakura, ni kushindwa kutimiza wajibu wa msingi wa uwakilishi. Wajibu huo, unajumuisha kusikiliza na kufuatilia maslahi ya waliomchagua. Hali hii inaweza kujitokeza kwa dalili mbalimbali zikiwemo tano.

**Dalili ya kwanza** ni Mbunge kutowasiliana na wapigakura. Jambo hili linakuwa dhahiri kwa Mbunge ambaye haitishi mikutano au hatoi mrejesho wa kazi anayoifanya Bungeni, wala hasikilizi changamoto za wananchi.

**Dalili ya pili** ni Mbunge kutoonekana jimboni. Hili linasababisha kujitokeza kwa maoni kwamba, Mbunge hafiki jimboni na wala hafanyi uchambuzi wa mahitaji ya jamii. Vilevile, Mbunge anaacha kushirikiana na viongozi wengine au wadau katika kuchochea maendeleo.

**Dalili ya tatu** ni Mbunge kushindwa kuwasilisha hoja za wapigakura wake Bungeni. Hali hii inaonekana kwa Mbunge kutoshiriki mijadala inayogusa maslahi ya jimbo lake wala kutouliza maswali yanayolenga majibu kuhusu changamoto za msingi zinazowakabili wapigakura wake. Dalili hii inapaswa kuchukuliwa kwa umakini ikizingatiwa kwamba, kuna njia mbalimbali za kuwasilisha hoja ama kwenye Kamati ambapo ni vikao vya ndani, njia ya kuwasilisha hoja kwa maandishi ambayo hayasomwi Bungeni au kuunganisha na hoja nyingine yenye mwelekeo wa kutoa ufumbuzi kwa jambo la Jimboni.

**Dalili ya nne** ni Mbunge kupuuza malalamiko, maombi au maoni ya wananchi. Dalili hii ni kwa Mbunge anayekuwa mbali na wananchi kiasi kwamba wapigakura wake hawajisikii kuwa na mwakilishi.

**Dalili ya tano** ni Mbunge kuwakilisha maslahi yake binafsi au ya makundi maalumu badala ya maslahi ya umma. Hali hii inaweza kujitokeza kwa Mbunge anayejiingiza katika vitendo vya upendekeleo, rushwa au migongano ya maslahi kinyume na matarajio ya wapigakura.

Kwa ujumla, dalili zozote za Mbunge kutowajibika kwa wapigakura wake zinaonesha kushindwa kwa Mbunge huyo kutekeleza jukumu lake la msingi la uwakilishi. Wapigakura, kwa vyovyote wasingaliweza kumchagua Mbunge ambaye wana uhakika kwamba, angalishindwa kuwajibika kwao.

**Pili ni uwajibikaji kwa Bunge lenyewe**. Kanuni ya 170 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2025 inampa Mbunge wajibu wa kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake. Kwa mujibu wa Kanuni hii, kuhudhuria vikao na kushiriki kikamilifu kwa kufuata Kanuni za Kudumu za Bunge ni wajibu wa Mbunge unaosisitizwa kuwa wa kwanza. Kwa Kanuni hiyo, kutohudhuria na kushiriki vikao vya Bunge na Kamati zake ni kutotimiza wajibu wa kwanza. Athari yake ni Mbunge kushindwa kutimiza wajibu wake katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge.

Madhara ya Mbunge kutowajibika kwa Bunge ni pamoja na kudhoofisha utendaji wa Bunge, na Kamati za Bunge pamoja na wananchi kukosa mwakilishi madhubuti. Ikitokea wabunge wengi hawawajibiki kwa Bunge inavyostahili, kutakuwa na athari hasi kwa taswira ya Bunge. Wananchi watapoteza imani kwa chombo chao cha uwakilishi na hadhi ya Bunge itashuka.

**Tatu ni uwajibikaji kwa Chama chake cha siasa**. Mbunge anawajibika kuheshimu misimamo ya Chama chake cha siasa. Misimamo hiyo ni pamoja na sera za Chama, mitazamo ya Chama na nidhamu ya Chama cha siasa cha Mbunge. Mzee Pius Msekwa, Spika Mstaafu baada ya Bunge la Nane la Tanzania alieleza kwamba, Mbunge anao wajibu kwa Chama chake cha siasa kwa sababu amepata ubunge kupitia Chama hicho.

Maana ya Mbunge kutowajibika kwa Chama chake

**"Uwajibikaji wa Mbunge kwa dhamiri yake ni uwajibikaji wa ndani, unaoamuliwa na nia yake, misingi ya maadili na utu wa Mbunge mwenyewe. Mbunge anayetawaliwa na nia thabiti, haongozi kwa hofu, shinikizo au matarajio ya kisiasa, bali kwa kile anachojua kuwa ni sahihi na cha heshima kwa wananchi aliooamua kuwatumikia."**

ni kushindwa kuwakilisha, kuheshimu na kutekeleza matakwa, misimamo, maadili na sera za Chama kilichompa ridhaa ya kugombea hadi kupata ubunge. Hili litaonekana kwa Mbunge kwa dalili tano bayana.

Dalili ya kwanza ni Mbunge kupuuza maadili, miongozo na taratibu za Chama. Dalili ya pili ni Mbunge kutukuonesha nidhamu kwa Chama chake cha siasa ikiwemo kutokuheshimu uongozi wa Chama. Na dalili ya tatu ni Mbunge kutojishughulisha na shughuli za Chama katika eneo analowakilisha au kitaifa kwa utaratibu wa Chama hicho.

Aidha, dalili ya nne ni Mbunge kutokutoa taarifa sahihi kwa Chama chake kuhusu shughuli zake za kibunge. Zaidi ya dalili hizo, ipo dalili nyingine ambayo ni Mbunge kutanguliza maslahi yake binafsi mbele ya maslahi ya Chama chake anapotekeleza majukumu yake.

Kwa ujumla, kutowajibika kwa Chama ni kushindwa kuwakilisha, kuheshimu na kutekeleza matakwa, maadili na sera za Chama cha siasa kilichompa ridhaa hadi kuwa Mbunge. Madhara yake ni kuchukuliwa hatua za kinidhamu ndani ya Chama, kupoteza uaminifu wa Chama, kudhoofisha uwezo wa Chama kusukuma ajenda Bungeni, kupoteza imani ya wapigakura na kuathirika kwa uwakilishi.

**Nne ni uwajibikaji kwa nchi yake**. Aina hii ya uwajibikaji ni uzingatiaji na utekelezaji wa wajibu wa Mbunge wa kikatiba, kijamii na kizalendo. Wajibu huo unamtaka Mbunge kutekeleza majukumu yake kwa kuchochea maslahi ya taifa, kulinda Katiba, kusimamia matumizi ya rasilimali za umma na kuhakikisha Serikali inafanya kazi kwa uadilifu, ufanisi na kwa manufaa ya wananchi wote. Dalili za uwajibikaji huu zinajumuisha mambo saba.

La kwanza ni Mbunge kuweka maslahi ya taifa mbele ya maslahi binafsi au siasa na jambo la pili ni Mbunge kuchangia kutungwa kwa sheria bora. Jambo la tatu ni Mbunge kusimamia ipasavyo utekelezaji wa shughuli za umma kupitia Bunge na Kamati za Bunge na la nne ni Mbunge kutetea haki, ustawi na usalama wa watanzania. Jambo la tano na la sita ni Mbunge kuhakikisha kwamba bajeti na sera zinawanufaisha wananchi pamoja na Mbunge kudumisha umoja, amani na maadili ya kitaifa.

Jambo la saba ni Mbunge kukosa mwelekeo unaoendana na dira ya kitaifa. Hili linatokana na Mbunge kutoelewa masuala ya kimkakati ya taifa. Mfano mwelekeo wa taifa kuhusu uchumi, nishati, diplomasia, uwekezaji, mazingira na mengine kadhaa. Aidha, Mbunge anatamalaki katika utoaji wa hoja zisizo na misingi au zisizolingana na maslahi ya taifa.

Kwa kifupi, maana ya Mbunge kuwajibika kwa nchi yake ni kufanya uamuzi, kuchukua hatua na kuwa na mwenendo unaozingatia maslahi mapana ya taifa na sio maslahi binafsi au maslahi ya kichama. Wakati wote Mbunge anaposhiriki katika uamuzi anakuwa na wajibu wa kuzingatia maslahi ya taifa, uadilifu, utawala bora, usimamizi wa rasilimali na ustawi wa wananchi. Mambo hayo yanamfanya Mbunge kuwa mtoaji wa hoja za kina, mwenye ushiriki kamilifu katika shughuli za Bunge na Kamati zake, mzingatiaji wa maadili, mfuatiliaji wa rasilimali na mteteaji wa maslahi ya taifa.

**Tano ni uwajibikaji kwa dhamira yake mwenyewe**. Maana yake ni uwezo wa Mbunge kujiweka kwenye viwango vya juu vya maadili, uadilifu, uwazi na utumishi uliotukuka bila kulazimishwa na Bunge, Chama chake cha siasa au wananchi. Ni uwajibikaji unaotokana na msimamo wa ndani wa kimaadili, unaomwongoza Mbunge kufanya yaliyo sahihi, kulinda hadhi ya Ofisi yake na kuweka kipaumbele kwa maslahi ya taifa na wananchi kwa hiari yake mwenyewe.

Kwa kifupi, uwajibikaji wa Mbunge kwa dhamiri yake ni uwajibikaji wa ndani, unaoamuliwa na nia yake, misingi ya maadili na utu wa Mbunge mwenyewe. Mbunge anayetawaliwa na nia thabiti, haongozi kwa hofu, shinikizo au matarajio ya kisiasa, bali kwa kile anachojua kuwa ni sahihi na cha heshima kwa wananchi aliooamua kuwatumikia.

Dalili saba za uwajibikaji wa Mbunge kwa dhamiri yake ni Mbunge kujiepusha na rushwa na kutojihusisha na mivutano isiyona manufaa, kuongozwa na ukweli na maslahi ya taifa wakati wa kupiga kura ya uamuzi na kukubali makosa na kuchukua hatua za kujirekebisha. Dalili nyingine mbili ni Mbunge kujikita kwenye kutoa taarifa za ukweli mahali sahihi kuhusu shughuli na matumizi ya rasilimali za umma, kuwa na nidhamu ya kazi ambayo maana yake halisi ni Mbunge kujenga hoja kwa misingi ya ukweli bila lengo la kupotosha.

Dalili ya sita na ya saba ni Mbunge kuwa na ushiriki unaofaa kwenye shughuli za Bunge bila udanganyifu na kukataa upendeleo au zawadi zinazolenga kumfanya apuuze maslahi ya umma badala yake kusimamia ukweli na maslahi ya taifa.

Kwa kujumuisha, makala hii imebainisha kwamba, **uwajibikaji wa Mbunge** ni nguzo kuu ya ufanisi wa Bunge na msingi wa uhalali wa kisiasa, uwakilishi na utawala wa kidemokrasia. Kwa ujumla, ufa-



fanuzi umeonesha kuwa uwajibikaji wa Mbunge ni uwezo wake wa kusimamia majukumu yake ya kikatiba, kijamii na kimaadili kwa kutoa maelezo, kufafanua na kutoa majibu kuhusu hatua, uamuzi wa kibunge na mwenendo wake.

Fauka ya hayo, makala imeainisha aina au namna tano za **uwajibikaji wa Mbunge** zinazotokana na uhusiano alionao Mbunge na wahusika wengine. Uhusiano huo ni baina yake na **Wapigakura**, na **Bunge lenyewe** na **Chama chake cha siasa**, na **nchi yake** pamoja na uhusiano wake wa kibunge na **dhamiri yake mwenyewe**. Kwa kuzingatia hayo, Tanzania ina Kanuni za Bunge na Sheria mbalimbali zinazotumika kuwafanya Wabunge watekeleze wajibu wao bila kushindwa kwa makusudi, kwa uzembe au kwa hiari.

Kuelekea kwenye hitimisho, jambo la kuondoka nalo ni kuwa, uwajibikaji wa Mbunge si suala la kuchukuliwa kama desturi ya hiari, bali ni mfumo mpana unaohusisha maadili, utendaji, uwazi na utumishi wa umma. Ni dhana yenye kujengwa juu ya uhusiano wa uwakilishi kati ya Mbunge na Wapigakura, uhusiano wa kisiasa kati yake na chama chake, wajibu wa kikatiba kwa Bunge na taifa na uadilifu wa ndani ya nafsi yake unaomdhibiti kama kiongozi.

Hivyo, uwajibikaji wa Mbunge ni mkusanyiko wa vitendo, mienendo na misimamo inayojenga imani, inayoendeleza demokrasia, inayoongeza ubora wa uamuzi wa kibunge na inayoweka msingi wa Bunge lenye uwezo wa kuisimamia Serikali kwa ufanisi. Yote hayo yana nafasi muhimu katika kuimarisha heshima ya Bunge.

Mwisho ikumbukwe kuwa, uwajibikaji wa Mbunge ni kigezo muhimu cha kupima afya ya mfumo wa uwakilishi na mustakabali wa demokrasia ya nchi. Uadilifu wa Mbunge mmoja mmoja huakisi taswira ya Bunge zima na hujenga ama kuvunja imani ya wananchi kwa vyombo vyao vya kikatiba. Kwa hiyo, ili Bunge liendelee kuwa chombo madhubuti cha kusimamia Serikali na kuwatumikia wananchi, ni lazima kila Mbunge achukue kwa uzito wajibu akizingatia kuwa dhamana aliyopewa ni ya taifa na kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Ufafanuzi zaidi kuhusu uwajibikaji wa Mbunge utaendelea kutolewa katika Toleo lijalo. Ikumbukwe kuwa walisema wahenga wenye kusema *"Aliyesikia nusu ya maneno, asikose kurudi kusikia yaliyobaki."* Hivyo, kwa kuwa mjadala kuhusu uwajibikaji wa Mbunge ni mpana na endelevu, ni mwaliko kwa wasomaji kuendelea kufuatilia toleo lijalo ili kupata ufafanuzi mpana zaidi na kuyaunganisha kwa ukamilifu masuala yote muhimu ya dhana hii.




# Diplomasia ya Kibunge yaimarishwa kupitia Mkutano wa 68 wa CPC na Mkutano wa 151 wa IPU

*Na. Debora Sanja*

**Katika kuendeleza juhudi za kuimarisha diplomasia ya kimataifa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard ameshiriki mikutano miwili mikubwa ya kimataifa.**

**Mikutano hiyo ni Mkutano wa 68 wa Mabunge Wanachama wa Jumuiya ya Madola (CPC) uliofanyika Oktoba 5 hadi 12, 2025 Jijini Bridgetown nchini Barbados na Mkutano wa 151 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyia Oktoba 17 hadi 23,2025 Jijini Geniva nchini Uswisi.**

**Ushiriki katika mikutano hii umechangia kuongeza ushawishi wa Tanzania katika masuala ya kikanda na kimataifa, sambamba na kuboresha mifumo ya kibunge nchini.**

Mkutano wa 68 wa Mabunge Wanachama wa Jumuiya ya Madola ulihudhuriwa na zaidi ya Wabunge 500, Makatibu wa Mabunge na wadau mbalimbali ukiwa na kauli mbiu "Jumuiya ya Madola – Mshirika wa Kimataifa."

Pamoja na kujadili masuala ya utawala na maendeleo, mkutano uliweka msisitizo katika kuimarisha diplomasia, kukuza haki za binadamu, kutetea demokrasia, na kufikia malengo ya kujenga taasisi imara za kidemokrasia kwa vizazi vijavyo.

Katika Mkutano huo pamoja na mambo mengine uliidhinisha Mpango Mkakati wa CPA 2026–2029.

Mpango huo unalenga kulinda misingi ya kidemokrasia, kukabili changamoto za kimataifa na kutoa mwongozo wa ushirikiano kwa ajili ya kujenga mabunge thabiti, yenye uwajibikaji na yanayozingatia maslahi ya wananchi.




**Ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya CPC, IPU na ASGP unaendelea kuonesha dhamira thabiti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha diplomasia ya kibunge, kuimarisha demokrasia na kusimamia utawala bora**

Mada kuu za majadiliano zilihusu mkakati wa kujenga mijadala bila chuki na migawanyiko pamoja na mabadiliko ya tabianchi na wajibu wa mabunge katika kusimamia ulinzi wa mazingira.

Mada nyingine ni matumizi salama na yenye maadili ya teknolojia na akili bandia (AI) katika shughuli za Bunge, kusaidia nchi ndogo na za visiwa (SIDS) kukabili athari za tabianchi na kukuza ushiriki wa wanawake, watu wanaoishi na ulemavu na vijana katika uongozi wa kibunge.

Mkutano wa 68 ulimalizika tarehe 10 Oktoba 2025, huku Mkutano wa 69 ukipangwa kufanyika Afrika Kusini mwaka 2026.

Kwa upande wa Mkutano wa 151 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) ambao ulihudhuriwa pia na Katibu wa Bunge, uliwakutanisha wawakilishi kutoka zaidi ya mabunge 130 duniani.

Kauli mbiu ya mkutano ilikuwa kuheshimu misingi ya kibinadamu na kuunga mkono hatua za msaada katika nyakati za migogoro."

Ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 151 wa IPU pamoja na mambo mengine umechangia kuimarisha nafasi ya nchi katika majadiliano ya kimataifa na kukuza diplomasia ya kibunge na kuongeza ushawishi wa nchi katika masuala ya kimataifa.

Mkutano huo pia umewezesha kubadilishana uzoefu katika kuimarisha kamati za Bunge, mafunzo ya wabunge na watumishi, pamoja na mifumo ya utawala bora.

Kupitia majadiliano haya, Tanzania imenufaika na mbinu mpya na maarifa yatakayosaidia kuboresha utendaji ndani ya Bunge, hivyo kuongeza mchango wa Bunge katika maendeleo ya wananchi.

Wakati wa Mkutano wa 151 wa IPU kulifanyika pia Mkutano wa Chama cha Makatibu wa Mabunge (ASGP) kuanzia tarehe 20 hadi 22 Oktoba, 2025.

Mkutano huu uliwaleta pamoja Makatibu wa Mabunge kutoka nchi mbalimbali kujadili masuala nyeti ya uendeshaji wa mabunge.

Mada zilizojadiliwa zilijumuisha mbinu bora za kuwaandaa viongozi watarajiwa (leadership succession planning), kuboresha mifumo ya kiutendaji na usimamizi wa rasilimali watu na kuongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za kibunge.

Katika mkutano huo, Bunge la Tanzania lilitambuliwa kuwa miongoni mwa mabunge yanayofanya vizuri katika kuwashirikisha vijana, kupitia Kitengo Mawasiliano na Elimu kwa Umma ambacho huendesha programu za elimu kwa wanafunzi.

Ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya CPC, IPU na ASGP unaendelea kuonesha dhamira thabiti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha diplomasia ya kibunge, kuimarisha demokrasia na kusimamia utawala bora.

Kupitia majukwaa haya ya kimataifa, Tanzania inaendelea kujenga nafasi imara katika diplomasia ya kimataifa, kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kuchochea ustawi na maendeleo endelevu ya wananchi.

Tanzania pia inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 153 wa IPU mwaka 2026 uliopangwa kufanyika Jijini Arusha.

# Umuhimu wa Kamati za Bunge katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge

**Na**. Athuman Hussein, *ndc*

a.brambati@bunge.go.tz

Safu hii inahusu mambo mbalimbali juu ya umuhimu wa Kamati za Bunge na ni mwendelezo kutoka matoleo yaliyotangulia. Miongoni mwa matoleo hayo ni toleo la kumi ambalo lilikuwa na nukuu ya Prof. Gavin Dewry, msomi mashuhuri wa masuala ya utawala wa umma na taratibu za kibunge wa nchini Uingereza. Nukuu hiyo ilikuwa ni "Kwenye Kamati ndiko ambako kazi halisi ya Bunge [*The real work of Parliament*] inapofanyika".

Serikali Bungeni ulikuwa nje ya Kamati za Kudumu za Bunge. Wakati huo, Bunge lilikuwa na Kamati za aina mbili: Kamati za Matumizi za Kisekta na Kamati za Kudumu kama ilivyoelezwa awali.

Kamati zilizoshughulikia bajeti ni Kamati nane tu ambazo ni Kamati za Matumizi za Kisekta. Hizo ziliundwa tangu mwaka 2001 na kuendelea kuwepo hata kwa mabadiliko ya Kanuni ya mwaka 2002. Uanzishwaji wa Kamati hizo ulilenga kuwa na Kamati mahsusi kwa

> **Mwaka 2003 mabadiliko ya kimfumo na kimuundo wa Kamati za Kudumu za Bunge yaliendelea kutokea. Idadi ya Kamati za Kudumu za Bunge iliongezeka kutoka nane (8) hadi kumi na tano (15). Majukumu ya Kamati mahsusi kwa ajili ya uchambuzi wa bajeti za Wizara yalijumuishwa kwenye majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge kumi na nne (14).**

Nukuu hiyo ililenga kusisitiza umuhimu wa Kamati za Bunge katika kutekeleza madaraka ya Bunge. Msisitizo huo pia ulitaka kupata usuli wa umuhimu wa Kamati za Bunge la Tanzania kihistoria. Kwa mantiki hiyo, mfumo wa Kamati za Bunge ulifafanuliwa kwa kuzingatia mabadiliko ya idadi, majina ya Kamati, utaratibu na uhusiano miongoni mwa Kamati za Bunge. Hayo yote yalielezwa kwa mtazamo wa kihistoria tangu mwaka 1961 hadi mwaka 2002.

Katika toleo hili ufafanuzi unaendelezwa kwa kuangalia mwaka 2003 hadi 2007 na kuegemea kwenye nukuu ileile. Ikumbukwe kwamba, mfumo wa Kamati za Bunge Tanzania haukuibuka ghafla. Ni mfumo ambao uliendelea kujengwa na kukuzwa kulingana na mabadiliko mbalimbali ya kikatiba, kisiasa na kisheria nchini, ndani ya kanda za Afrika au duniani kwa ujumla.

Hadi mwaka 2002 utaratibu wa Bunge kutunga sheria na kuisimamia Serikali ulifanyika chini ya Kamati za Kudumu za Bunge. Lakini uchakataji wa bajeti ya ajili ya uchambuzi wa bajeti kama ilivyoainishwa na Kanuni ya 81 (1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2002. Maisha ya Kamati hizo yalikuwa ni kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wa Bunge.

Aina ya pili ya Kamati za Bunge wakati huo ni Kamati za Kudumu za Bunge ambazo kwa idadi, zilikuwa kumi na tatu. Hivyo, jumla ya Kamati za Bunge zilizokuwepo mwaka 2002 ni Kamati ishirini na moja (21), yaani nane (8) za kisektana kumi na tatu (13) za kudumu. Wakati huo, Kamati za Kudumu za Bunge zote zilipewa jukumu la kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni ambazo zinagusa mambo yote yaliyo chini ya mamlaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge inayohusika kama ilivyobainishwa katika Kanuni ya 90 (1), toleo la 2002.

Mwaka 2003 mabadiliko ya kimfumo na kimuundo wa Kamati za Kudumu za Bunge yaliendelea kutokea. Idadi ya Kamati za Kudumu za Bunge iliongezeka kutoka nane (8) hadi kumi na tano (15).

Majukumu ya Kamati mahsusi kwa ajili ya uchambuzi wa bajeti za Wizara yalijumuishwa kwenye majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge kumi na nne (14).

Mabadiliko hayo yaligusa idadi ya jumla ya Kamati za Bunge. Ikilinganishwa na mwaka 2002, mfumo wa Kamati za Bunge kwa mwaka 2003 ulibadilika kwa namna ya wazi kwenye maeneo makuu matatu (3).

Eneo la kwanza ni idadi ya jumla ya Kamati. Mabadiliko yalikuwa ni kupungua kwa idadi ya Kamati za Bunge kutoka ishirini na moja (21) hadi kumi na tano (15). Mwaka 2002 mfumo wa Kamati za Bunge ulikuwa na Kamati ishirini na moja (21) lakini kwa mabadiliko ya mwaka 2003, Mfumo wa Kamati za Bunge ukawa na Kamati kumi na tano (15) za Kudumu za Bunge.

Eneo la pili ni kwenye majukumu ya Kamati za Bunge. Mfumo wa Kamati za Bunge kwa mwaka 2002 uliweka majukumu ya Kamati za Bunge katika kategoria mbili tofauti. Kategoria hizo ni majukumu ya uchambuzi wa bajeti za Wizara na majukumu ya usimamizi wa kawaida wa kibunge. Majukumu ya kushughulikia bajeti za matumizi ya wizara yalipangwa kisekta chini ya zilizokuwa Kamati za Bunge za Kisekta za Matumizi. Kwa upande mwingine, majukumu ya usimamizi wa kiBunge wa kawaida yalielezwa chini ya Kamati za Kudumu za Bunge.

Eneo la tatu linahusu kuanzishwa kwa Kamati mpya. Mabadiliko ya mwaka 2003 yalianzisha Kamati mbili mpya katika mfumo wa Kamati za Kudumu za Bunge. Kamati hizo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi.

Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu yalikuwa ni kufuatilia na kushughulikia masuala ya miundombinu nchini. Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa upande wake, ilipewa jukumu la kufuatilia masuala ya ardhi, maendeleo ya makazi, kilimo na chakula, maji, na maendeleo ya mifugo.

Eneo la nne ni kwenye sura ya kimuundo ya Kamati tatu za Kudumu za Bunge kwa maana ya jina na wigo wa majukumu yake. Mabadiliko hayo yaligusa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma, Kamati ya Mazingira na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Makundi Mengine Maalumu.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma ilichukua sura mpya na kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara. Kwa sura hiyo mpya,msukumo mkubwa kwenye kazi za Kamati za Bunge uliwekwa kwenye kufuatilia inavyostahili suala la mazingira ya biashara nchini.

Msisitizo wa ufuatiliaji wa mitaji ya Umma ulipungua kutokana na kuongeza mkazo kwenye mazingira ya biashara. Mtaji wa Umma katika muktadha huu ni maslahi ya umiliki wa Serikali na mali za kifedha (*financial assets*) zilizowekezwa katika mashirika ya Umma, kampuni au miradi. Kwa ujumla ni sehemu ya utajiri wa taifa unaomilikiwa na Serikali na inatarajiwa kuzalisha faida za kiuchumi au kijamii.

Kwa upande wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mazingira, mabadiliko yalihusu kuongezeka kwa wigo hadi kwenye usimamizi wa kibunge wa shughuli za umma zilizohusu utalii. Mwaka 2002 suala la utalii halikupewa msisitizo bayana kwenye jina la Kamati yoyote, lakini mwaka 2003 msisitizo ulianza kujitokeza kwenye jina na majukumu ya Kamati.

Kamati nyingine ni Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Makundi Mengine Maalumu. Mabadiliko ya wigo wa majukumu yake kwenye jina yaliongezeka. Badala ya kuishia kwenye usimamizi wa shughuli za umma zinazohusu wanawake na makundi mengine maalumu, wigo ulifika hadi kwenye maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Jambo lingine lililojitokeza katika mfumo wa Kamati za Bunge ni kuhusu jukumu la kushughulikia taarifa za hesabu zilizokaguliwa. Katika kipindi hicho Kamati zilizokuwa zinasimamia shughuli za umma za wizara, zilihusika pia na kufuatilia hesabu zilizokaguliwa na mashirika ya Umma chini ya Wizara zinazohusika.

Eneo la tano, ni jukumu la kuchambua sheria ndogo lililokuwa chini ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Katiba na Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 93 (2) (c) ya Kanuni za Bunge,za mwaka 2002. Mabadiliko ya Kanuni ya mwaka 2003 yalidondosha jukumu la uchambuzi wa sheria ndogo kwa kuchanganya majukumu ya iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Utawala na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Katiba na Sheria.

Mwaka 2004, Bunge lilifanya mabadiliko ambayo hayakuwa makubwa na bayana kwenye mfumo wa Kamati za Kudumu za Bunge. Maeneo yaliyoguswa zaidi ambayo ni ya jumla ni suala la upeperushaji wa bendera na makatazo ya kukashifu bendera ya Bunge. Jambo hilo halikuwa sehemu ya mfumo wa Kamati za Bunge.

Kufuatia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutawala wa Nchi, mwaka 2007 Bunge lilifanya mageuzi katika utaratbu wake wa kutekeleza madaraka yake. Mageuzi hayo yaligusa pia mfumo wa Kamati za Bunge.

Mambo manane (8) makuu yaliyoguswa yanastahili kuelezewa.

**Jambo la kwanza** katika mabadiliko ya mwaka 2007 ni uanishaji wa Kamati katika kategoria. Kategoria hizo ni Kamati Zisizo za Kisekta, Kamati za Kisekta na Kamati zinazosimamia Matumizi ya Fedha za Umma. Uainishaji huo ulilenga pamoja na mengine, mambo manne (4).

Kwanza, ni kuepusha mkanganyiko na utata wa majukumu. Hili lilifanyika kwa kuonnesha bayana majuku-

mu tofauti yanayoweza kutambuliwa kwenye kategoria moja na kutofautishwa na kategoria nyingine.

Pili, ni kurahisisha uratibu wa kazi kutokana na mpangilio unaoeleweka wa aina za Kamati za Kudumu za Bunge. Hali hii inarahisisha uendeshaji na kuongeza ufanisi wa Bunge katika kutekeleza madaraka yake kupitia kazi za Kamati za Bunge.

Tatu, ni kuwezesha ufanisi wa kiutawala na kiuratibu. Inakuwa hivyo kwa kuwa kila kategoria inajulikana inavyohusika na mambo maalumu ambayo hayazihusu Kamati za kategoria tofauti. Kuimarika kwa masuala ya utawala na uratibu wa shughuli za Kamati kunaongeza tija ya kazi za Kamati na kukuza ufanisi wa Bunge.

Nne, ni kujenga uwezo wa Kamati kwa urahisi kutokana na Kamati zilizo kwenye kategoria moja kuwa na malengo yanayoendana na wakati mwingine utaalamu na mbinu zinazoendan au kuchukuana. Uwezo huo ni muhimu kwa ufanisi wa Bunge katika utekelezaji wa madaraka yake.

Kwa ujumla mfumo wa Kamati za Kudumu za Bunge usipokuwa kwenye kategoria unaweza kusababisha mkanganyiko. Kwa maneno mengine utachangia ugumu katika uratibu wa kazi za Kamati na kupunguza ufanisi wa uratibu katika azma ya kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge.

**Jambo la pili** katika mabadiliko ni kuhusu idadi ya Kamati. Kabla ya mabadiliko ya mwaka 2007 jumla ya Kamati za Kudumu za Bunge ilikuwa Kamati kumi na tano, lakini mwaka 2007 zikawa Kamati kumi na nane. Idadi hiyo ilizingatia mpangililo wa utekelezaji wa Shughuli za Umma unaofanywa na Serikali.

**Jambo la tatu** ni dhana kuu mbili (2) zilizopata uzito wa kipekee katika majukumu ya Kamati. Kwanza ni dhana ya Kamati kulisaidia Bunge kusimamia utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka zingine. Kamati iliyohusika ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya sheria ndogo iliyopewa jukumu la kuchambua sheria ndogo zote.

Pili ni dhana ya usimamizi wa kibunge wa masuala ya UKIMWI. Badala ya suala la UKIMWI kusimamiwa kama ambavyo masuala mengine ya afya yalivyosimamiwa, lilipewa msukumo mahsusi kwa kuwa wakati huo duniani na katika kanda ya kusini mwa afrika, Bunge lilikuwa ni chombo kilichokuwa na jicho la kipekee kwenye janga la UKIMWI na VVU. Kamati hiyo ilijulikana kama Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI.

Kamati zote mbili (2): Kamati ya Kudumu ya Bunge ya sheria ndogo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI zilikuwa ni Kamati mpya na zilianzishwa katika mfumo wa Kamati za Bunge kwa mara ya kwanza mwaka 2007. Majukumu yaliyowekwa chini ya Kamati hizo, awali yalikuwa yakitekelezwa na Kamati tyofauti katika vipindi mbalimbali vya historia ya Kamati lakini bila kuwepo kwa Kamati mahsusi. Hii inaonesha kuwa jicho la kipekee la Bunge na msisitizo maalumu uliwekwa katika mfumo wa Kamati za Bunge kwa mabadiliko ya mwaka 2007.

Pamoja na Kamati hizo mbili (2) mpya, Kamati ya tatu(3) mpya ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Kabla ya mwaka 2007, mfumo wa Kamati za Kudumu za Bunge haukuwa na Kamati maalumu kwa ajili ya kufuatilia shughuli za umma zinazotekelezwa katika sekta ya nishati na madini.

**Jambo la Nne** lilikuwa kwenye eneo la usimamazi wa matumizi ya Fedha za Umma kwenye mashirika ya umma kabla ya mwaka 2007, suala hili halikuwa mahsusi kwenye Kamati maalumu. Kamati mbalimbali zilifuatilia hesabu za mashirika ya umma yaliyo chini ya Wizara zinazosimamia.

Kuanzia mwaka 2007, mfumo wa Kamati za Bunge uliainisha Kamati zinazosimamia Matumizi ya Fedha za Umma katika kategoria moja. Kamati hizo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ambayo ni kongwe, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) iliyotokana na historia ya PAC na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma iliyokuwa mpya.

**Jambo la tano** ni kuchanganywa kwa majukumu ya Kamati zilizokuwa zinasimamia masuala ya ulinzi na usalama na masuala ya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa. Kwa sababu hiyo, iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Us-

**Jambo la sita lilihusu uendeshaji wa Kamati za Kudumu za Bunge.**

Kabla ya mwaka 2007 suala la Kamati kualika wadau katika dhana ya ushirikishaji na ushughulishaji wa Umma kwenye masuala ya kibunge liliwekwa kwenye utungaji wa sheria, pale ambapo Kamati ilipewa jukumu la uchambuzi wa miswada ya sheria. Kwa wakati huo, Kanuni hazikuweka sharti la lazima kwa Kamati inayoshughulikia muswada wa sheria kushirikisha watu wengine au wadau. Kanuni ya 69 (2) ya Kanuni za Bung za mwaka2004 ilitoa hiari kwa Kamati kualika watu. Mabadiliko ya mwaka 2007 yaliweka sharti la lazima katika Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mwaka 2007 na kuongeza njia za mwaliko ambazo ni barua au matangazo ya mwaliko.

alama ziliondoka katika mfumo wa Kamati za Kudumu za Bunge. Badala yake ilianzishwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, maarufu kwa jina la (NUU). Kamati hii ilipewa majukumu ya Kamati mbili zilizoondolewa kwenye mfumo wa Kamati za Bunge.

**Jambo la sita** lilihusu uendeshaji wa Kamati za Kudumu za Bunge. Kabla ya mwaka 2007 suala la Kamati kualika wadau katika dhana ya ushirikishaji na ushughulishaji wa Umma kwenye masuala ya kibunge liliwekwa kwenye utungaji wa sheria, pale ambapo Kamati ilipewa jukumu la uchambuzi wa miswada ya sheria. Kwa wakati huo, Kanuni hazikuweka sharti la lazima kwa Kamati inayoshughulikia muswada wa sheria kushirikisha watu wengine au wadau. Kanuni ya 69 (2) ya Kanuni za Bung za mwaka2004 ilitoa hiari kwa Kamati kualika watu. Mabadiliko ya mwaka 2007 yaliweka sharti la lazima katika Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mwaka 2007 na kuongeza njia za mwaliko ambazo ni barua au matangazo ya mwaliko.

Zaidi ya hivyo, wigo wa sharti la kualika wadau uliongezeka chini ya masharti ya Kanuni ya 114 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,mwaka 2007. Wigo huo uligusa shughuli zote za kawaida za Kamati ambapo iliwekwa kuwa sharti muhimu kwa Kamati kualika wadau ili kupata maoni na ushauri wao kwa ajili ya kuboresha jambo linaloshughulikiwa na Kamati.

**Jambo la saba** lilihusu katazo kwa mjumbe wa Kamati kuzungumzia au kushughulikia jambo lolote lililofikishwa katika Kamati iwapo atakuwa na maslahi binafsi katika jambo hilo au idara hiyo. Sharti hili liliwekwa chini ya Kanuni ya 114 (19) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mwaka 2007. Kwa mujibu wa Kanuni hiyo Mbunge anayeweza kuzungumzia jambo hilo baada ya kutaja jinsi inavyohusika na kiwango cha maslahi aliyonayo.

**Jambo la nane** ni nia ya Bunge kudumisha mahusiano na wananchi kupitia vyombo vya habari kwa kuwezesha upatikanaji wa habri kutoka kwenye vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge. Nia hiyo ilijitokeza katika Kanuni ya 114(19) na 114(10) za Kanuni za Bunge ambazo zilifafanuliwa katika Nyongeza ya Saba ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mwaka 2007. Kanuni hizo na nyongeza yake, zilitoa mwongozo wa mambo ya uwazi, mambo yafaragha na namna habari zinavyoweza kupatikana.

Mabadiliko hayo pia yalilenga kukuza demokrasia ya kibunge na uwazi wa shughuli za Kamati. Lengo hilo lilielezwa katika kifungu cha 1 cha Nyongeza ya Saba ya Kanuni za Kudumu za Bungmwaka .

Kuelekea katika hitimisho, inakumbushwa kwamba, matoleo yaliyotanguliwa yaligusa mambo mbalimbali kuhusu umuhimu wa Kamati za Bunge. Matoleo hayo pia yalifafanua historia ya mfumo wa Kamati kuanzia mwaka 1961 hadi 2002. Toleo hili limebainisha historia ya mfumo wa Kamati za Bunge kwa kipindi cha kati ya mwaka 2003 na 2007. Mambo mengi yamebainishwa kutokana na historia. Inawezekana kabisa mambo hayo yanaarifu uzoefu unaosaidia kuelewa umuhimu wa Kamati za Bunge.

Kwa msingi huo, kauli ya mwanafalsafa mtajika, Aristoto ambaye ni mwanafunzi wa Plato, inayotanabahisha kwamba, "Ili kuelewa jambo lolote, chunguza mwanzo wake na maendeleo yake''. Kauli hiyo inathibitishwa na mambo yanayojitokeza katika historia ya Kamati za Bunge kwa kipindi kilichofafanuliwa.

Katika toleo lijalo, ufafanuzi utaendelezwa ikiwemo kuonesha historia ya Kamati za Bunge kwa kipindi cha 2007 hadi sasa. Kufuatilia toleo lijalo ni sehemu ya jitihada muhimu za kupata uelewa wa masuala ya Bunge kwa uhakika. Tukumbuke kauli ya wahenga, hususan wa Pwani ya Afrika Mashariki wasemao "**Ukilima pantosha, utavuna pankwisha**."



Jarida hili limeandaliwa na: Ofisi ya Bunge, 10 Barabara ya Morogoro S.L.P. 941, 40490 Tambukareli, DODOMA.
Nukushi: +255 26234218 Simu: +255 26 232276-5 Barua Pepe: cna@bunge.go.tz